# ALIYE MKUU KULIKO SULEMANI YUPO HAPA

Asante, sana.

2 Hebu tuendelee kusimama kwa muda kidogo tu, tafadhalini, tunapomwendea Mungu katika maombi. Tunapoinamisha vichwa vyetu sasa, mbele Zake, sijui kama kuna haja yoyote maalum tungetaka ijulikane na Mungu kwa mkono ulioinuliwa, nawe uinue mkono wako, moyoni mwako useme, "Mungu, nikumbuke juu ya jambo *fulani*."

3 Baba yetu wa Mbinguni, ni majaliwa makuu, usiku wa leo, kuja na kusema "Baba" kwa Muumba wa Mbingu na nchi, tukijua ya kwamba Yeye anatujali sana hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na Uzima wa Milele. Tunashukuru sana, usiku wa leo, ya kwamba tumeamini, na tumepokea Uzima wa Milele kwa imani yetu katika Yeye.

4 Sasa, tuna haja nyingi miongoni mwetu, usiku wa leo, Baba. Umeona kila mkono, unajua kila sababu ya mkono huo kuinuliwa, jibu, Baba. Ninaweka maombi yangu pamoja na yao madhabahuni, imani yangu pamoja na yao, na kuomba kwamba Mungu mwenye rehema atatujalia haja hiyo, tunaposihi juu ya Dhabihu iliyojaa Damu, Bwana Yesu Kristo.

5 Sasa, bariki ujumbe, usiku wa leo, na uwabariki watu walio hapa kuupokea, wabariki wale wanaoutoa. Pia jalia Roho Mtakatifu awe na haki ya kuingia katika kila moyo. Jalia tuondoke hapa usiku wa leo, tukiwa na furaha na kushangilia, na kusema, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, tulipokutana katika Uwepo Wake tena?" Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

6 Mwaweza kuketi. Nina furaha sana kweli, tena usiku wa leo, kuwa hapa, na baada ya jana jioni, na wakati mzuri sana pamoja na Bwana, nilikuwa na ushirika mzuri sana jana usiku kwenye Neno la Mungu. Nilikuwa nikila kiamshakinywa asubuhi ya leo pamoja na mtu fulani, nasi tulikuwa tukilizungumzia, na mara nikakutana na mtu mwingine na, mtu fulani aliyekuwa kwenye mikutano, nao wakasema, "Ndugu Branham, nilikuwa kwenye mikutano yako ya awali, ulipoanza kwa mara ya kwanza, yapata miaka kumi na mitano iliyopita, huku kwenye Pwani ya Magharibi."

7 Ilikuwa hapa chini kwenye Santa—Santa Rosa, ninaamini, ni huko. Santa Rosa? Na usiku mmoja kule, kulikuwa na muungwana akijaribu kuingia kwenye mstari wa maombi, na

mhudumu mmoja alikuwa pamoja nami wakati huo, ambaye anachukua. . . alikuwa. . . Billy alikuwa. . . amechukua mahali pake. Alikuwa. . . angesambaza kadi za maombi, na kuweka mstari sawa. Na loo, jamani, watu wangeendesha magari maili elfu moja kwa teksi wapate tu kufika mkutanoni.

8 Naye akaendelea kutaka. . . Bw. Brown alikuwa amemwondosha kwenye mstari wa maombi mara mbili au tatu, hakuwa na kadi ya maombi, naye ananinii. . . Nilimsikia akisema, "Vema, nilitaka tu kuzungumza naye."

Na kwa hiyo nikasema, "Ni kitu gani, bwana?"

Akasema, "Nilitaka tu kujua jinsi unavyoendeleza jina lako la mwisho."

Nami nikasema, "B-r-a-n-h-a-m."

Naye akasema, "Ndilo hilo, Mama," kisha akaenda na kuketi chini.

Nami nikawaza, "Vema, sasa, ajabu hiyo. Kwa nini aombe kitu kama hicho?" Nikasema, "Naweza kuuliza. . . ?"

9 Akasema, "Vema, bwana, yapata miaka ishirini na mitano iliyopita, wakati Pentekoste ilipokuja kwa mara ya kwanza kwenye Pwani ya Magharibi," akasema, "mimi na mke wangu tulipokea kipawa cha Roho." Mmoja wao angenena kwa lugha na huyo mwingine angetoa tafsiri. Nao ulitoa unabii, nao wakauandika.

10 Kisha kasema, "Usiku wa leo, nilipokuja nyumbani, nilikuwa nikisoma gazetini makala ya wewe kuwa hapa Santa Rosa." Akasema, "Nami nikamwambia mke wangu, 'Mpenzi, hilo kidogo si linasikika linalojulikana kwako kwa namna fulani?'" Na hao watu huenda wako wameketi sasa hivi kwa yote nijuayo. Kasema, "'Hilo si linasikika. . . ?'"

Kasema, "'Loo, vema,'" kasema, "'gazeti limekuwa likimtangaza mhudumu huyu.'"

Kisha kasema—kasema, "'Lakini hilo linasikika linalojulikana.'"

11 Na baada ya chakula cha kutwa, walipanda darini na kuchukua ninii ya kale. . . huko juu upenuni, kisha wakatoa sanduku hili la nguo, ama kitu fulani cha kale walimobebea unabii wao. Kipande cha kale cha karatasi ya manjano, na mmoja wao alikuwa amenena kwa lugha, na huyo mwingine alikuwa ametabiri Nao ukasema, "BWANA ASEMA HIVI: Itakuwa, kabla tu ya wakati wa mwisho kwamba mtumishi Wangu, William Branham, atakuja huku Pwani ya Magharibi akiwaombea wagonjwa." Na kwa hiyo. . . Naye akasema imeandikwa "W-i-l maradufu i-a-m B-r-a-n-h-a-m." Na hiyo hapo, karatasi ya kale ya manjano ya miaka ishirini na mitano kabla ya hapo, nami ningekuwa na yapata umri wa miaka saba

au minane, hiyo ingekuwa yapata mwaka wa 1915, mahali fulani hapo, mnaona, ambapo ilitendeka.

12 Nayo Pwani ya Magharibi ina kumbukumbu nyingi muhimu kwangu. Nami daima ninaenda kwenye Pwani hii ya Magharibi. Kwa nini? Ustaarabu umesafiri pamoja na jua. Ustaarabu wa kale sana tulio nao uko mashariki, na huko ndiko Roho Mtakatifu aliposhuka kwa mara ya kwanza, ilikuwa huko mashariki. Nao ustaarabu umesafiri kuelekea magharibi, na umefika kwenye Pwani ya Magharibi, maili moja ama mbili tu upande huu, ama hivyo, nadhani, nasi tuko—tuko baharini, tunarudi moja kwa moja mashariki tena. Hapa ndipo lundo lote la kila kitu limepigapiga, hapa kwenye Pwani hii ya Magharibi, huku. Huku ndiko mema na mabaya, yaliyo mabaya kuliko yote na mazuri kuliko yote, yanapokutana, papa hapa kwenye Pwani ya Magharibi.

13 Kabla sijaondoka Pwani ya Magharibi wakati huu (Huenda hii ndiyo safari yangu ya mwisho ya kimishenari hapa na pale huku.), na, ni—ninataka kuhubiri juu ya *Wakati Mashariki Na Magharibi Zinapokutana*. Nami nimekuwa na kitu kama muktadha moyoni mwangu kwa muda mrefu.

14 Nilikuwa nikimwambia mtu huyu aliyesema, "Ndugu Branham, ulipokuja, ilikuwa tu ni karama ndogo, kila baada ya muda fulani mstarini, ungemshika mtu fulani, na kuushika mkono wao, na kusimama hapo kwa dakika chache, na kuwaangalia machoni na kusema, 'Una ugonjwa *fulani*,' na daima ilikuwa sahihi.

15 "Lakini ulitabiri, nawe ukasema wakati utakuja, ambao Malaika wa Bwana alikuwa amekwambia, ambaye alikuwa amekuagiza uende, aliyekuagiza uende, ambapo utajua siri za moyo wao, na ungewaambia watu mambo waliyokuwa wamefanya, na wangefanya, na kadhalika. Ulitabiri hilo lingetimia."

16 Kisha kasema, "Huduma yako, leo hii, iko juu asilimia mia moja na zaidi kuliko ilivyokuwa wakati huo, maana kila kitu ulichotabiri kingetimia, kimetimia, na huduma yako ni kuu zaidi." Kasema, "Ulisimama jana usiku kwa mwanamke mmoja, chini mstarini," kasema, "ukasimulia tu historia yake, kile kilichokuwa kinaendelea." Kisha kasema, "Watu walionekana kusema, 'Hilo ni zuri sana.'"

17 Kisha kasema, "Ni kwamba tu, wakati ungewashika watu mkono mara ya kwanza, na kusema tu jambo moja, watu wangekimbilia madhabahuni upesi walivyoweza." Kisha kasema, "Ulifanya wito wa madhabahuni jana usiku," ndipo kasema, "kulikuwa na watu walioketi pale?"

18 Nikasema, "Waliorudi nyuma, wenye dhambi, na kadhalika," mnaona, na kusema, "hakuna hata mtu mmoja angejibu." Nikasema, "Mnaona," mnaona, "karama za Mungu

zimekamilishwa, bali uamsho umekwisha kwa muda mrefu." Mnaona? Uamsho umekwisha, 1956 nilitabiri huko Chicago ya kwamba Billy Graham, mwaka huo angerudi na kufutilia mbali mikutano yake, Tommy Osborn angerudi, nayo Marekani ingeona wito wake wa mwisho, na tangu wakati huo uamsho ungekufa. Sasa, hesabuni tu nyuma mwone. Tuna hayo kwenye kumbukumbu. Mnaona? Nao uamsho umekwisha.

19 Mnaona, nuru haina budi kuninii...Maji hayana budi kuangukia Mbegu iliyo na Uzima, la sivyo haitakuwa Hai. Hakuna Uhai mle wa kuifanya Hai, "Wote alionipa Baba watakuja. Wala hakuna mtu awezaye kuja, asipoitwa na Baba Yangu." Mnaona? Hiyo—hiyo ni kweli. Kwa hiyo leo hii... Uamsho umekwisha.

20 Huduma ya Oral Roberts, ninakumbuka mara ya kwanza nilipokutana na Oral Roberts, maskini hema lililochakaa akiketi upande ule mwingine, nilikuwa katika—katika Jiji la Kansas, Missouri, uh, Kansas, naye alikuwa katika Jiji la Kansas, Missouri. Tulikutana nyuma ya jukwaa, akanisalimia kwa mkono, naye akasema, "Ndugu Branham, unafikiri Mungu angejibu maombi yangu kwa ajili ya wagonjwa?"

21 Nikasema, "Yeye hujibu maombi ya mtu yeyote kwa ajili ya wagonjwa." Nasi tukapigwa picha pamoja, ziko katika nakala ya kale ya *Sauti Ya Uponyaji* kama...wengi wenu mnayo, labda. Na hapo—hapo ndipo Oral alipoanzia.

Angalieni jinsi huduma yake imepanuka, na sasa kufikia mamilioni na mamilioni na mamilioni ya dola, sasa anajenga shule kubwa mno ya theolojia.

22 Ninawazia juu ya Billy Graham, papa hapa chini Los Angeles wakati *Vijana Kwa Ajili Ya Kristo* wote walipoanza kumwombea, jinsi ambavyo magazeti yaliandika kumkosoa, yalimkosoa kwa kusema si—simba, Leo, alimpiga teke tumboni na kusema, "Angalia kama huyo ni mnene wa kutosha kulaza kichwa chake mle." Kwa hiyo, wazia mhudumu kusema jambo kama hilo. Leo, wangeogopa kusema jambo hilo, lakini Billy Graham, huduma yake imepanuka pakubwa sana. Mnaona?

23 Huduma ya Oral Robert imepanuka. Ile karama ndogo ambayo Mungu alinipa na kutabiri, angalieni jinsi ilivyopanuka. Mnaona? Lakini hata hivyo, uamsho unakufa, unakufa, unakufa.

24 Billy Graham alisema huko Louisville, wakati alipokuwa... mji wangu wa nyumbani, naye aliketi pale, nilikuwa kwenye kiamshakinywa chake cha wahudumu, akasema, "Ninaenda mjini, nami nitakuwa na mkutano humo wa majuma sita, na kupata thelathini elfu" (Anayaitaje? Maungamo? Ama maamuzi.) "maamuzi elfu thelathini." Kasema, "Narudi katika miezi sita, siwezi kupata thelathini."

25 Akasema, "Paulo aliingia mjini, naye akapata uamuzi mmoja kwa ajili ya Kristo, akarudi mwaka mmoja baadaye

na kupata thelathini ama arobaini kutoka kwa huyo mmoja." Kasema, "Sasa, kuna shida." Hakika. Mnaona?

26 Wakati tu uamsho unapoanza, naye Roho wa Mungu anatenda kazi, Mungu anatenda kazi pamoja na watu, ndipo akiliondoa zao hilo, akaliondoa kabisa, haya basi, hilo ni kwa ajili ya kizazi hicho. Pia kumbukeni, Yeye alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ambapo watu wanane waliokolewa, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu." Mnaona? Kila kizazi kitazaa tu *kiasi fulani*. Na hivyo ndivyo unavyoliona siku hizi, kila mahali, ni kufa tu, kuanguka. Dhambi inaporomokea kila kitu.

27 Tumekuja kwenye mikutano, wataninii . . . Nilikuwa kwenye mkutano huko chini Los Angeles juma lililopita kwenye uwanja wa maonyesho kule, ambapo mahali hapo palikuwa pamejaa umati mkubwa wa watu. Nao wote walionekana kumpenda Bwana, lakini ilionekana kana kwamba u—uko karibu tu kwisha. Fanya wito wa madhabahuni, na kwa kweli, usingeweza kumleta mtu yeyote madhabahuni, hakuna mtu.

28 Na unapoufanya, wao kwa kweli si Wakristo. Wao ni . . . Jinsi walivyo, (ninamaanisha wenye kukiri tu.), wao ni watu ambao wakati mmoja wamemjua Bwana, na wamerudi tu nyuma, nao wanarejea. Kwa hiyo huko si . . . tusingeweza kuwaita waongofu, wameongoka hapo walipomkubali Kristo. Walianguka tu, wanaufanya tu upya ushirika wao. Mnaona? Lakini waongofu, hakuna dazani moja kwa mwaka, nadhani, karibu, hasa katika—katika mikutano yetu midogo. Kwa hiyo, mnaona, karibu tu masazo yote yameokotwa mashambani.

29 Lakini hata hivyo, ukuu wa Mungu kuhakikisha ya kwamba kila mmoja ameshikwa, kila chembe imehifadhiwa, hata vile vipande vilivyosalia kwenye vile vikapu kumi na viwili vinaokotwa. Mnaona? Mungu haachi chochote . . . Yeye huchambua huku na huko kondeni tena apate kuyashika tena. Hivi si tunashukuru kwamba tuna Baba kama huyo?

30 Sasa, usiku wa leo . . . Jana usiku nilisema, "Tutawaachilia mtoke, saa tatu na nusu," saa nne kabla sijatoka. Kwa hivyo sikuzote mimi huchelewa. Mwajua, mama yangu aliniambia nilikuwa mtoto wa miezi tisa kamili. Kwa kweli nilichelewa kidogo kufika hapa, na sikuzote nimechelewa.

31 Hapa wakati fulani uliopita nilikuwa nikihubiri kwenye kanisa la United Brethren, nami nilikuwa nimechelewa yapata saa moja. Kwa hiyo huyo mhudumu, alipofika kwenye kusanyiko lililokuwa linangojea, limesimama kuzunguka kuta, alisema, "Sasa ninamtambulisha kwenu *mchelewaji* Bw. Branham." [Katika Kiingereza, 'the late' inaweza pia ikawa na maana ya 'marehemu'.—Mfa.]

32 Nilipofunga ndoa mke alilazimika kuningojea yapata saa moja na nusu, nilimkalisha pale kwa muda mrefu. Laiti

ningeweza tu kuchelewa kwenye mazishi yangu! Hilo ndilo jambo linalofuata. Laiti ningeweza tu kukaa hapa muda mrefu vya kutosha kuchelewa kwa hayo, hivyo ndivyo ninavyotaka kuwa, kuchelewa sana kwa hayo.

33 Lakini wengine, mwajua, wanaweza . . . wanajua jinsi ya kulisema, na wasomi wenye elimu kujua jinsi ya kuliweka huko nje; nami ina—inanibidi tu kunyosha mkono na kulichukua na kuninii tu . . . Nami ninapenda kulifuatilia sana, hata sijui wakati wa kuacha kulifuatilia, mnaona. Na kwa hiyo, hiyo ndiyo njia pekee niliyo nayo ya kufanya jambo hilo, kwa hiyo nivumilieni kidogo.

34 Nami nina saa ya kengele hapa ambayo walinipa huko Uswisi, bali ninaona aibu tu kuifanya ilie wakati nikihubiri, mnaona. Kwa hiyo . . . Walinipa, nadhani hilo lilikuwa ni dokezo.

35 Lakini nilihubiri ma—mahubiri mafupi hivi majuzi huko, maskanini nyumbani, saa sita, saa sita tu. Msi—msiogope, sifanyi hivyo sasa, meneja wangu hapa nyuma angenivuta niondoke kabla ya wakati huo.

36 Hebu na tufungue, usiku wa leo, kwa usomaji wa Maandiko, katika Kitabu cha Mathayo Mtakatifu, mlango wa 12, na hebu tusome kidogo kwa ajili ya muktadha. Sasa, muda mfupi tulio nao, hebu na tuuweke kwa ajili ya Ufalme wa Mungu sasa. Mnaona?

37 Sasa, Bwana aliyaokoa maisha yangu siku chache zilizopita, ninyi nyote mmejua habari zake, wakati ile bunduki ilipolipuka usoni mwangu, mnaona. Nanyi mnaona kote machoni mwangu, na hizo alama na kadhalika, hapo ndipo We—Weatherby Magnum ilipolipukia usoni mwangu, na kulipua mtutu kwenye mstari wa yadi hamsini, na kukatilia mbali kila kitu kilichonizunguka, nao mwili wangu wote ungekatwa vipande viwili; karibu *hivyo* na jicho langu wakati nilipokuwa nikilenga shabaha kwenye uwanja wa shabaha.

38 Naye mtu aliyekuwa amesimama pamoja nami yuko ibadani, usiku wa leo, ameketi papa hapa nyuma akiniangalia. Angeokota tu miguu yangu, hivyo tu; wala haikunidhuru.

39 Ilidhoofisha . . . Vipande kumi na tano vilifanya duara ya nusu mwezi moja kwa moja chini ya macho, na kurudi moja kwa moja nyuma ya mboni ya jicho, *hili*, vikapita na kung'oa sehemu ya juu ya hili jino, na kunikata usoni, ndipo vipande vitatu au vinne vikachomekwa kwenye fuvu la kichwa na tezi za mapua, kote namna hiyo; kamwe haikunisumbua.

Kwa hiyo ilionekana kana kwamba aliyaokoa maisha yangu kwa sababu fulani, nami nipo hapa kuweka kila wakati moja kwa moja katika Ufalme wa Mungu.

Tunapoangalia, hebu nipate ninii kidogo . . .

40 Sasa, bunduki hiyo haikuwa Weatherby Magnum asili. Sikuzote nimetaka Weatherby Magnum. Kama mjuavyo, mimi huwinda wanyama wakubwa kote ulimwenguni. Nami sikuzote nimetaka moja, lakini kamwe sikuwazia ningeweza kununua moja. Halafu basi, baadhi ya marafiki zangu huenda wangeninunulia moja, lakini nisingeweza kuwaona wakilipa karibu dola mia tatu kwa ajili ya bunduki huku nina marafiki wamishenari wasio na viatu miguuni mwao, kwa hiyo ni—nisingefanya hivyo.

41 Naye Ndugu Art Wilson, hapa juu, akampa Billy Paul, mwanangu, maskini Winchester ya .257, mpya. Ndipo rafiki yangu aliye na kampuni ya Weatherby, ama, ni wakala wa Weatherby, kasema, "Ndugu Branham, naweza kuifanya bunduki hiyo itobolewe tena iwe Weatherby kwa kidogo sana ama bure tu." Kasema, "Naomba nifanye hivyo." Kasema, "Haitanigharimu zaidi ya dola kumi ama kumi na tano. Ni ninii. . .Hii hapa, moja kwa moja katika gazeti la *Weatherby*, imedhaminiwa."

Nami nikasema, "Vema, sawa," naye akaichukua.

42 Nami nilipaswa kujua vya kutosha kuhusu bunduki kujua ya kwamba nilipopiga mfululizo wa kwanza wa risasi kupata baruti, katikati tu ya mahali pa kuwashia na kichocheo cha nje pakafura. Nilipaswa kujua ilikuwa ikivuja pale, lakini sikupaona kamwe, nilifurahishwa sana na hiyo bunduki. Ndipo wakati mwingine nilipotia risasi ndani na kuivuta chini, ilizimika.

43 Nilijifunza somo pale, unaona. Unapokuwa Mkristo, au unapotaka kuwa Mkristo, usijipumbaze tu na upuuzi huu hapa wa kupeana mikono, huu hapa "wongofu wa ghafla," utalipukia mahali fulani barabarani. Sasa, kama hiyo ingekuwa ni Weatherby Magnum, *asili* yake iwe ni Weatherby Magnum, *ikatolewa* kama Weatherby Magnum, ingekuwa sawa, ingekuwa imeundiwa hiyo risasi. Lakini wakati unapojaribu kutia risasi kubwa inayoingizwa kwenye bunduki nyingine, katika kitu ambacho isingeweza kustahimili! Unaona?

44 Kama unataka kuwa Mkristo, zaliwa mara ya pili, ufe kwa nafsi yako, uanzie chini ndipo ujitokeze, hakutakuwa na milipuko njiani, uta—uta—utaweza kushikilia chaji ambayo Roho Mtakatifu anatia ndani yako. Hiyo ni kweli. Usipofanya hivyo, kamwe hutaweza kuistahimili, hivyo tu. Bwana awabariki.

45 Hilo ni jambo fidhuli kusema, sivyo? Lakini natumaini mnapata kile ninachozungumzia. Ninaamini ya kwamba inakupasa kufa sana hata isiwe ni wewe tena, hivyo tu, na halafu, uzaliwe upya tena, kiumbe kipya katika Kristo, kilichojengwa kutoka ndani kabisa ya nafsi yako kote kote, Mkristo halisi aliyezaliwa mara ya pili. Ndipo Roho Mtakatifu

atajua aina ya mzigo wa kuweka ndani yako. Hiyo ni kweli. Utaweza kuubeba.

46 Ukijaribu kumwiga mtu mwingine kuwa Mkristo, utalipukia mahali fulani, kutakuwa na mlipuko mahali fulani ndani yake. Usijaribu kuiga, kuwa bidhaa halisi ya Mungu, ama usiwe, kaa tu jinsi ulivyo, unaona, hiyo ni kweli, kamwe usifanye maungamo yoyote. Vema.

47 Katika ninii . . . Mathayo m—mlango wa 12, kuanzia kifungu cha 38:

> *Hapo baadhi ya waandishi na Mafarisayo wakamjibu, wakasema, Mwalimu, twataka kuona ishara kwako.*
>
> *Akajibu, akawaambia, Kizazi kibaya na cha zinaa chatafuta ishara; wala hakitapewa . . . ishara, ila ishara ya nabii Yona:*
>
> *Kwani kama vile Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi; hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi.*
>
> *Watu wa Ninawi watasimama katika hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, . . . watawahukumu kuwa wamekosa: kwa sababu wao hawakutubu kwa mahubiri ya Yona; na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona.*
>
> *Malkia wa kusini atasimama . . . katika hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, naye atawahukumu kwamba wamekosa: kwa sababu yeye alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani; na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.*

Sasa, Bwana na aongeze baraka Zake kwenye kusomwa kwa Neno hili.

48 Yesu alikuwa akikemea kizazi hicho. Kama ukisoma sehemu iliyotangulia ya hicho kifungu, kifungu kilichotangulia, walikuwa wameita ishara aliyokuwa amewapa (Ishara ya Kimaandiko kwamba Yeye alikuwa ni Masihi. Tulilizungumzia jana usiku.), nao, walikuwa wameitangaza kuwa ni Beelzebuli, mpiga ramli, ibilisi. Jambo lile lile walilomwona akifanya, hao Mafarisayo, sasa, kamwe hawakulisema moja kwa moja moyoni mwao . . . midomoni mwao, waliliwazia mioyoni mwao, wa—walijisemea moyoni mwao, "Yeye ni Beelzebuli, mkuu wa pepo."

49 Naye Yesu alijua walichokuwa wanawazia, Naye akawaambia, akasema kwamba, dhambi hiyo, wakati Roho Mtakatifu alipokuja kufanya ishara ile ile ambayo Yeye alikuwa ametoa, neno dhidi Yake lisingesamehewa kamwe. Alikuwa ameiambia ile miji . . .

50 Jambo la kuchukiza sana lililopo, enyi marafiki, ni kutokuamini, hiyo ndiyo dhambi pekee iliyopo; hakuna dhambi nyingine ila kutokuamini. Nilikuwa nikihubiri juu ya hilo miaka kadhaa iliyopita katika kanisa la Kimethodisti. Lilikuwa ni kanisa zuri, kubwa la Kimethodisti, na—nao, wengi wao, ama, baadhi yao, wanaamini katika utakatifu, Wamethodisti wa kusini. Nao walikuwa. . . Nami nilikuwa nikihubiri kuhusu. . . Nikasema, "Kufanya uzinzi sio dhambi," nikasema, "kusema uongo sio dhambi, kulichukua Jina la Bwana sio dhambi."

51 Hilo lilizidi sana kwa maskini dada mmoja mpendwa aliyeketi pale, huku ukosi wake umeinuliwa kote, akasema, "Naomba uniambie, dhambi ni nini?" Hiyo ni kweli. Asingeweza kuvumilia tena.

52 Nami nikasema, "Dhambi, dhambi ni hii, dada yangu, unaona, dhambi ni kutokuamini. Wanafanya mambo haya, wanafanya uzinzi, wanasema uongo, na wanafanya mambo haya, ni sifa za kutokuamini. Kama wangalikuwa ni waaminio, wasingefanya mambo hayo. Hiyo ni. . . wao ni wasioamini, hiyo ndiyo sababu wanafanya hivyo. Ni sifa tu zinazothibitisha ya kwamba wao ni wasioamini. Kwa kuwa Yesu, Maandiko yanatufundisha waziwazi ya kwamba "asiyeamini amekwisha kuhukumiwa." Mnaona? Hata huwezi kuanza. Kwa hiyo jambo baya sana lililopo, ni kutokuamini.

53 Ni kwa nini watu wanasema, "Siku za miujiza zimepita"? Maana wao ni wenye dhambi.

54 Mtu fulani alikutana nami si muda mrefu uliopita, kasema, "Sijali utafanya nini, na ungeweza kuonyesha mathibitisho mangapi, bado siamini katika uponyaji wa Kiungu."

55 Nikasema, "Haukutolewa kwa ajili ya wasioamini, ulitolewa tu kwa ajili ya waaminio." Hiyo ni kweli. Mnaona? Ni kwa wale tu wanaoamini, si wasioamini, hawana—hawana nafasi. Wala u—usiwakosoe, bali wazia tu juu ya hali hiyo waliyomo maskini watu hao. Unaona?

56 Yesu alisema, "Mna macho, wala hamwezi kuona. Mna masikio, hamwezi kusikia," na hata hivyo ni wasomi hodari sana katika dini, waalimu na wanatheolojia wa siku hiyo. Yesu alisema, "Enyi Mafarisayo vipofu mkiwaongoza vipofu." Mnaona? Kwa sababu hawakumwamini Yeye, wakati Maandiko yalisema dhahiri ya kwamba hivyo ndivyo Masihi angekuwa. Nao wakamwita Ibilisi. Hiyo ni kweli. Mnaona? Wasioamini.

57 Yeye alisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu kwanza." Na hili hapa jambo la neema kulihusu: "Wote alionipa Baba watakuja." Hiyo ndiyo sehemu. Ninapenda hilo. Naam, bwana. "Wote alionipa Baba watakuja." Nami ninafurahia hilo. Kwa hiyo hatujui ni nani aliyeko na ni nani asiyeko, tunaisambaza tu hiyo Mbegu, hivyo tu ndivyo tunavyoweza kufanya, "zingine huanguka kando ya

njia; zingine zinaanguka *huku*, na *huko*; lakini zingine kweli huanguka kwenye udongo mzuri." Hiyo ni kweli, udongo ambao umeandaliwa na Mungu kuipokea Mbegu.

58 Ninawazia juu ya maskini mwanamke yule tuliyenena habari zake jana usiku, maskini yule kahaba. Jinsi maskini mwanamke huyo, akisimama pale katika hali aliyokuwamo, waume watano na akiishi na wa sita, na ni hali mbaya jinsi gani maskini mwanamke huyo aliyokuwamo! Na hata hivyo, kwa kweli mnajua alimjua Mungu zaidi kuliko kundi kubwa la makasisi wa Marekani hii? Hakika alijua, alijua mengi juu Yake kuliko kuhani mkuu na hao wengine wa siku zake, kwa kuwa walisema, "Huyo ni ibilisi."

59 Lakini mara hiyo Nuru ya Milele ilipoiangazia Mbegu hiyo iliyochaguliwa tangu zamani, ilikuwa Hai upesi sana. Waliiona, Wakaitambua upesi sana. Angalia hali aliyokuwamo, kulikuwa na makanisa mengi makubwa katika siku zake, mengi sana, hakuhudhuria lolote lao, alingojea tu, kwa sababu aliona kulikuwa na kitu fulani.

60 Lakini Biblia ilisema mpinga-Kristo katika siku za mwisho angewadanganya wote wakaao juu ya nchi, ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Mnaona? Sasa, hiyo hapo, na wakati Nuru hiyo ilipoiangazia njia ya maskini mwanamke huyo, aligeuka, wala hakusema, "Wewe ni Beelzebuli." Alisema, "Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii."

61 Ilikuwa ni kitu gani? Nuru hiyo ilikuwa imeishika, mara moja hiyo Mbegu ikawa Hai. Mnaona? Kitu fulani mle ndani, ndani yake, alikiona, alichaguliwa kukiona, aliitwa na Baba, alikuwa amepewa. . .ule Uhai ulikuwa umetolewa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Na mara hiyo Nuru ilipomwangazia, haidhuru ni kiasi gani cha mafunzo ya kikanisa kilichokuwa kimeonekana, wao hawakuiona, lakini wakati hiyo Nuru ya Mungu ilipommulikia maskini mwanamke huyo, aliiona.

62 Akasema, "Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii. Tunajua ya kwamba Masihi ajapo, Yeye atatwambia mambo haya." Hilo hapo. Mnaona? Haina budi kuwekwa mle ndani na Mungu na Yeye pekee.

63 Yesu alikuwa amewakemea, akasema, "Mnawezaje kuwa vipofu hivyo?" Akiwaambia, "Mngewezaje. . .kutokuamini kwe—kwenu. . .?"

Ndipo wakamjia, na baada ya haya yote, na ndipo wakasema, "Mwalimu, twataka kuona ishara kwako."

64 Hebu angalieni, Yeye alisema, "Kizazi kiovu na cha zinaa chatafuta ishara." Ni kizazi cha aina gani? "Kizazi kiovu na cha zinaa chatafuta ishara," nacho kitapata ishara, "wala hakuna ishara itakayopewa kizazi hicho kiovu na cha zinaa, ila ishara

ya Yona," Yona. Watapokea ishara ya Yona, kizazi kiovu na cha zinaa.

65 Hebu tusimame kwa dakika moja. Hakika alikuwa anazungumza juu ya kizazi *hiki*. Mnaona? Angalieni, mliwahi kuona ki—kizazi cha zinaa kama hiki? Labda ninyi, baadhi yenu huenda msijue, katika kusafiri kote ulimwenguni, hakuna wimbi kubwa la uhalifu wa uzinzi kuliko lililoko Marekani, ndiyo mbaya kuliko yote. Hata wana vilabu sasa, Los Angeles, Chicago ina vilabu kadhaa vikubwa, New York, ambako wote hukusanyika, nao wanaume wanatupa funguo zao kwenye kofia, ndipo mwanamke fulaini anaingiza mkono mle ndani na kuzichukua, huyo ndiye "mume" wake mpaka watakapokutana tena. Kiovu na cha zinaa!

66 Nilikuwa nikisoma gaze-. . . la Hollywood, ama, katika gazeti moja huku chini Los Angeles hapa, nilikuwa nimeruka juu ya Los Angeles hapa nje kwa mwaliko, nami nikachukua gazeti nilipokuwa nikiruka kwa ndege, nalo lilisema kwamba ushoga katika Pwani ya Magharibi ulikuwa umeongezeka, naamini, asilimia ishirini ama thelathini katika mwaka uliopita. Dhambi ya Sodoma! Kama Yeye alivyosema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa." Kiovu, cha zinaa!

67 Yote tunayoona, matangazo yetu ya televisheni, magazeti yetu, vibao vyetu vya matangazo, kila kitu kimejaa tu utovu wa adabu, uchafu, kinyaa, upotovu, wanawake nusu uchi. Ni fedheha. Na ni kwa nini? Hiyo ndiyo aina ya roho iliyo ndani ya watu wanaotamani hilo.

68 Ungewezaje kumwuzia mwanamke jozi ya maskini viatu vya vifungo kama mama alivyozoea kuvaa? Mbona, hata hivyo, vina ngozi kubwa zaidi kuliko jozi dazani moja wanavyovaa siku hizi, ngozi bora zaidi! Lakini usingeweza kupata senti hamsini kwa jozi ya hivyo, afadhali wapate kipande kidogo cha kitu fulani, na kulipa dola ishirini na tano kwa jozi moja kwa sababu kinaonekana kama cha jirani, ama nyota fulani wa Hollywood.

69 Wakristo hufanya hivyo pia. Ni aibu jinsi gani! Hatupaswi kuiga Hollywood. Hollywood hung'aa kwa uangavu na . . . lakini wakati Hollywood inang'aa katika—katika mng'ao na madoido, Injili inameka kwa unyenyekevu. Kuna tofauti kati ya kung'aa na kumeka.

70 Nayo makanisa yameanza kuang'aa kwa msomi hodari, na elimu, kanisa lililo kubwa kuliko yote, na *fulani-fulani*. Nao watu wetu wa full Gospel wanaingia moja kwa moja katika mtindo uo huo. Ni aibu. Humeka kwa unyenyekevu katika Kristo.

71 Sikutaka kuanza kuhubiri, nami nilisema katika mkutano huu nilikuwa ninaenda kusimama hapa na kuzungumza juu ya uponyaji wa Kiungu. Vema. Hebu na tulirudie. Vema.

72 "Kizazi kibaya na cha zinaa chatafuta ishara; nao watapokea ishara, ishara ya Yona." Sasa, "Yona alikaa katika

tumbo la, nyangumi siku tatu mchana na usiku; vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kukaa katika moyo wa nchi siku tatu mchana na usiku." Basi sikilizeni, jiletee mwenyewe, huenda ikawa ni nuru mpya juu ya Maandiko, huenda ikawa ni kitu fulani, lakini iko katika Maandiko: Ishara ya Yona ingekuwa ndiyo ishara ya ufufuo. Kizazi kiovu na cha zinaa kinachotafuta ishara, kitapata ishara ya ufufuo.

73 Sasa, tuna ufufuo kwa historia, lakini basi tuna ufufuo kwa ishara, ya kwamba Yesu Kristo yu hai, usiku wa leo, katika Kanisa Lake; Yeye hajafa, Yeye yu hai. Yohana Mtakatifu 14:12, Yesu alisema, "Yeye aniaminiye Mimi," kuna wengi, wanaokiri kuamini, bali Yeye alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya; nyingi kuliko hizi atafanya; kwa kuwa naenda kwa Baba."

74 Sasa, najua la King James linasema hapa, "kubwa zaidi," wasingeweza kufanya kubwa zaidi, Yeye aliwafufua wafu, akawaponya wagonjwa, akasimamisha maumbile, alifanya kila kitu, bali tafsiri sahihi ya Kiebrania cha asili, hata hivyo inasema, "*nyingi* kuliko hizi," kwamba, Kristo alikuwa katika Mtu mmoja pale, na Kristo yuko katika Kanisa Lake la ulimwenguni kote sasa, "nyingi ya kazi zile zile mtazifanya; kwa kuwa ninaenda kwa Baba Yangu. Bado kitambo kidogo na ulimwengu" kosmos, utaratibu wa ulimwengu, "hautaniona tena; bali ninyi mtaniona. Kwa kuwa Mimi," na *Mimi* ni kiwakilishi nafsi, kama nilivyosema, "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu," muda gani? "hata ukamilifu wa dahari." "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele."

75 Nuru za jioni zinaangaza, nao, kizazi hiki kinapokea ishara ya Yona. Yule Kristo waliyedhani wamemwondoa, kanisa lilimsulubisha Kristo miaka elfu mbili iliyopita, wala wasingeweza kumwua tena, Yeye alisema, "Mimi ni hai milele na milele," naye Huyu hapa, baada ya miaka elfu mbili, miongoni mwa watu Wake, akijionyesha Mwenyewe kwa mambo yale yale aliyofanya huko nyuma, anatenda papa hapa tena. Mnaona? Miaka elfu mbili imepita, Yeye yu hai milele, na ana funguo za mauti na kuzimu. Amina.

76 Nina furaha sana kwa jambo hilo. Loo, ingemfanya Mbaptisti apaze sauti! Hiyo ni kweli. Ninajisikia kubarikiwa sana sasa hivi, ninapowazia hilo. Liwazieni hilo, Yeye hakika yu hai, si mfu, yu hai.

77 Nilisema jambo dogo hapa si muda mrefu uliopita, linasikika la maana sana kwangu. Niliwaza juu ya Israeli huko chini Misri, watumwa, watu wa Mungu, watumwa. Ndipo siku moja, akishuka kutoka nyikani alikuja nabii akiwa na Nuru juu yake, naye akawaambia ya kwamba kulikuwako na nchi ya ahadi iliyojaa maziwa na asali. Hawakuwa wamewahi kuiona, hakuna mtu aliyekuwa amewahi kufika kule. Lakini walimwamini nabii

huyo, ilikuwa ni kulingana . . . unabii wake ulikuwa ni kulingana na Neno, nao wakamwamini.

78 Walimfuata mpaka wakafika mahali paitwapo Kadeshi-barnea, kiti cha hukumu cha ulimwengu. Kulikuwa na chemchemi moja kubwa yenye vijito kadhaa vidogo, ambavyo tungeweza kuingilia kwa undani kama tungalikuwa na wakati wa kuelezea hiyo ilikuwa ni nini, ambapo maji ya Uzima hutoka kwenye Kiti cha Enzi kwenda kwenye makanisa na kadhalika. Lakini ilikuwa ni hukumu, na Hukumu huanzia kwenye Nyumba ya Mungu.

79 Halafu basi, kwenye hii Kadeshi-barnea kulikuwako na mmoja kati yao aliyeitwa Yoshua, ambalo linamaanisha "Yehova-Mwokozi." Alivuka Yordani, ambako hakuna hata mmoja wao aliyekuwa huko hapo kabla, akaipeleleza hiyo nchi, na kurudisha ushahidi kwamba ilikuwa ni nchi tukufu, yenye ninii nzuri . . . iliyojaa maziwa na asali. Na kila kitu ambacho Mungu alikuwa ameahidi kilikuwa katika nchi hiyo kilikuwako, alirejesha huo ushahidi. Baada ya kuvuka mto Yordani, hakuna mtu aliyewahi kuwa kule, akarudi, "Mbona, kuna—kuna zabibu zinazokua!" Watu wawili walibeba kishada kimoja. "Ni mahali pa jinsi gani Yehova ametupa sisi! Maneno Yake ni kweli." Hawakutaka kuamini hilo, hata hivyo wawili wao, Kalebu na Yoshua, waliutuliza umati wakati wakiielezea.

80 Hatimaye wakavuka Yordani, wakairithi hiyo nchi. Haikuwabidi kuwa watumwa, binti zao walibakwa, wana wao wakauawa kwenye . . . na tanuri za kuokea, au katika mashimo ya matope, na kadhalika, chini ya watawala wakatili wa Misri, yenye giza. Haikuwabidi kufanya hivyo tena. Wangeweza kuwa na miti yao wenyewe, wangeweza kukuza shamba lao wenyewe la mizabibu, wangeweza kuwalea watoto wao katika amani, mataifa mengine yaliwaheshimu. Jinsi ningetaka kuingilia hilo, mfano wa taifa hili!

81 Ndipo muda si muda mwajua, kilichotukia, baada ya kitambo kidogo wakazeeka, wakaanza kufa. Makaburi yakawa kando ya kilima cha nchi hiyo tukufu, na haidhuru Mungu alikuwa ameyabariki vipi, bado iliwabidi kufa.

82 Ndipo akaja Shujaa mwingine mkuu, akashuka kutoka Utukufuni, Jina Lake lilikuwa ni Yesu wa Nazareti, Mwana wa Mungu. Akawaambia ya kwamba ipo Nchi ambamo mtu hafi, kwamba kuna Uzima baada ya mauti. Hakuna mtu aliyewahi kuwa Huko bado na akarudi. Naye akaja kwenye Kadeshi-barnea Yake, Kalvari, ambako hakustahimili tu hukumu, kiti cha hukumu cha ulimwengu, bali ulimwengu ulihukumiwa pale, Yeye alilipa adhabu ya dhambi zetu pale Kalvari.

83 Baada ya Kalvari alivuka kile tunachokiita Yordani ya mauti. Siku ya tatu akafufuka tena, akirudi kutoka kwenye Nchi

ile, akileta ushuhuda ya kwamba mtu, anapokufa, huishi tena. Tuko hai. Amina. Ha—haitubidi kuchukua . . .

84 Sasa, Yeye alisema, "Nitawapa Arabuni ya hii, niwape Ushahidi wake, lakini ngojeni huko juu kwenye mji wa Yerusalemu mpaka nitakapowapelekea Ushahidi kwamba Nchi hiyo ni nzuri, Nchi hiyo inawaweka huru na dhambi."

85 Na sasa, leo, baada ya miaka elfu mbili, tungali tunasimama na Arabuni ya wokovu wetu, ule Ushahidi, kuangalia chini na kuona mahali tulipokuwa wasioamini wakati mmoja, ambapo wakati mmoja tulikuwa wafu katika dhambi na makosa, na sasa tumefufuka pamoja Naye katika ufufuo. Tulikufa pamoja Naye, tukafufuka pamoja Naye, nasi tumeketi, usiku wa leo, katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu, tayari tumefufuka pamoja Naye katika ufufuo, amina, huku kila kitu kikiwa chini ya miguu yetu. Amina. Magonjwa, mauti, kuzimu, vyote vimeangamizwa na Shujaa wetu mkuu, ambaye tunasimama karibu na mkono Wake wa kuume. Amina.

86 Hofu ya nini? Si ajabu mmoja wao alikuja na kusema, "Mauti, u wapi uchungu wako? Kaburi, u wapi ushindi wako? Mungu na ashukuriwe, atupaye ushindi kwa Bwana wetu Yesu Kristo. Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, imani nimeilinda. Na kuna taji niliyowekewa ambayo Bwana, Hakimu mwenye haki, atanipa Siku ile, si mimi tu, bali na wale wote wanaopenda kuonekana Kwake." Amina.

87 Vipi kama Yeye angaliishi katika siku hii? Siwezi kukaa na somo langu, usiku wa leo, kwa namna fulani. Sasa, walikuwa wakimhukumu, Yeye alikuwa amewaonyesha ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi. Maskini mwanamke huyo kahaba, alisema, "Bwana," kwa maneno mengi ili tuweze kuelewa, "hiyo ndiyo ishara atakayofanya Masihi." Nao hawakuamini hilo. Mnaona?

88 Sasa, Yeye alisema, "Kutakuwako na kizazi cha zinaa kitakachotafuta ishara; nao wataipata, na itakuwa ni ishara ya Yona. Kama vile alivyokuwa katika tumbo la nyangumi, kisha akafufuka tena kwenye . . . kutoka kwenye tumbo la nyangumi baada ya siku tatu; Mwana wa Adamu atafufuka tena."

89 Bila shaka, msomaji yeyote wa Maandiko anajua ya kwamba Maandiko yote yana jibu maradufu, unabii wote. Chukua somo lako la pambizoni, kama "Kutoka Misri nimemwita Mwanangu," Mathayo 2, uone kama hiyo hairejei kutoka Misri Yeye alimwita Yusufu. Unaona? Yusufu alikuwa Mwanawe, na vivyo hivyo Yesu Mwanawe; daima lina maana mbili. Kwa hiyo basi, hicho pia, kizazi hicho hakikuamini ishara ya ufufuo kwa Msamaria na Myahudi pia.

90 Na sasa, hili hapa tena, baada ya miaka elfu mbili ya misukosuko ya kikanisa, na vurugu, na kadhalika, ndipo tena ishara hiyo ya Masihi inaonekana miongoni mwetu, nao

wangali wanageuza vichwa vyao, wanasema, "Nadhani ni sawa." Mnaona? "Kizazi kiovu na cha zinaa kitatafuta ishara," nao wataipata.

91 Mwajua, watu wengi sana sikuzote wanamhukumu maskini Yona wa kale, yeye alikuwa ni nabii, kasema alikuwa nje ya mapenzi ya Bwana. Nitamtetea kwa muda kidogo, siamini ya kwamba nabii huyo alikuwa nje ya mapenzi ya Bwana. Ninaamini Biblia ilisema ya kwamba "mambo yote hufanya kazi pamoja kwa manufaa ya wale wampendao Mungu." Mtu huyo aliyasalimisha maisha yake kwa Mungu, na kujaribu kufanya kazi . . . kutembea katika nyayo za Mungu, Mungu hufanya kila kitu kitembee sawa, uh, kitende kazi vizuri kwa ajili yake. Kweli.

92 Tunaona Yona . . . Bila shaka, Mungu alimwambia aende Ninawi, mji ule mkubwa yapata ukubwa wa St. Louis, Missouri, huko kote katika . . . wote katika ibada za sanamu. Waliabudu wanyama, na mu—mungu wa bahari alikuwa nyangumi, na—nao walikuwa na miungu ya kila namna. Waovu, uzinzi, mambo ya kila namna yalikuwa yakiendelea, mpaka dhambi zao hata zikaja mbele za Mungu. Naye akamtuma nabii huyu kule chini kuzikemea dhambi zao.

93 Sasa, kama nabii huyo alishuka kwenda kule kuninii tu, katika siku hizo na kupaza sauti dhidi ya dhambi, hao watu wangalimcheka na kuondoka, kwa hiyo Mungu akamfanya achukue meli hiyo nyingine. Naye akachukua merikebu yake, akaenda, badala ya kwenda Ninawi, anaenda Tarshishi. Alipokuwa akienda zake kule, dhoruba ikatokea, tunajua Biblia, nao wakamfunga mikono na miguu wakamtupa nje, ndipo nyangumi akammeza.

94 Sasa, najua walimleta nyangumi huko Louisville, mifupa ya mmoja, kwenye—kwenye mkokoteni si muda mrefu uliopita, naye mtu huyo alikuwa akitoa hotuba, kasema, "Sasa," kasema, "mara nyingi mmewasikia wahudumu wakisema ya kwamba—ya kwamba nyangumi huyu alimmeza Yona." Kasema, "Angalieni hapa, mpira wa miguu usingeweza kupitia kooni mwake." Akasema, "Hiyo inaonyesha ya kwamba hiyo hadithi ya Biblia ilikuwa ni hekaya."

95 Hilo lilizidi sana kwangu, nikangojea tu mpaka nikapata nafasi yangu, nikasema, "Bwana, ningetaka kukwambia jambo fulani. Unasema hivyo kwa sababu huijui Biblia." Nikasema, "Mungu alisema alimweka tayari samaki. Huyu alikuwa ni wa aina tofauti." Hiyo ni kweli. "Alikuwa na koo kubwa vya kutosha Yona angaliweza kuruka ndani yake." Unaona? Nikasema, "Huyo alikuwa ni nyangumi maalum aliyeandaliwa na Mungu." Mungu alimwandaa samaki. Naam, bwana. Alimfanya mkubwa vya kutosha kummeza Yona.

96 Mungu hutimiza Neno Lake, sijali ni wakosoaji wangapi wasemao! Na kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu,

"Haitanyesha." Ilinyesha kwa vyovyote vile, Mungu alisema hivyo. Na yale Mungu asemayo, Mungu anaweza kuyatimiza.

97 Asemayo, Ibrahimu aliamini hivyo, na watoto wote wa Ibrahimu wanaamini hivyo. Na kama tukiwa ndani ya Kristo, sisi ni Uzao wa Ibrahimu na warithi pamoja naye, pamoja na ahadi. Ndipo inatubidi kuwa na imani aliyokuwa nayo Ibrahimu katika Neno la Mungu. Sawa. Hiyo ndiyo inayofanya mambo hayo yatimie, ni imani katika yale aliyosema.

98 Kamwe hutalisogeza kwa njia nyingine yoyote ila uwe na imani katika yale Mungu aliyosema. Huna budi kuliamini Neno Lake juu ya kila kitu kingine. "Neno la kila mtu na liwe uongo, na la Mungu liwe kweli." Alichosema Mungu, kiamini tu. Iwapo huwezi kukiamini hivyo, kamwe hutafika mahali popote na Mungu. Huenda ukaweza kujiunga na kanisa mahali fulani, ila ninamaanisha kufika mahali fulani na Mungu. Unaona? Hilo—hilo ni tofauti kabisa.

99 Sasa, tunaona ya kwamba nyangumi huyu alimmeza Yona. Halafu mtu yeyote anajua, ninyi akina dada mnaweza... ukimlisha maskini samaki wako wa dhahabu, anapolijaza maskini tumbo lake, anashuka moja kwa moja chini ya ule—ule mtungi mdogo ulimomtia, hicho chombo kidogo, ama chochote kile, anashuka huko chini, na kulaza maskini pezi zake moja kwa moja chini, na kupumzika, kwa sababu ameshiba. Ametembea-tembea majini mpaka akapata chakula, anapojaza tumbo lake, anashuka moja kwa moja na kupumzika.

100 Sasa, samaki huyu mkubwa, ambaye Mungu alimweka tayari, alijaza tumbo lake kwa nabii, kwa hiyo anashuka chini ya bahari kupumzika. Huenda ilikuwa ni kama mikono arobaini huko chini.

101 Na mara nyingi nimewasikia watu wakisema, "Niliombewa jana usiku. Angalia mkono wangu, ungali umelemaa." "Tumbo langu linauma vile vile tu." Daima litafanya hivyo pia. Unaona, unaangalia hizo dalili, usiangalie dalili, angalia Neno la Mungu.

102 Hapa siku moja, mzee mmoja wa thamani, yapata miaka kumi na mitano iliyopita, maskini ndugu mpendwa, alikuwa na mwana mmoja, na huyo mwana alikuwa yuafa, alikuwa na dondakoo nyeusi. Naye akaniomba, aliendelea kunisihi mchana na usiku nikamwombee mvulana huyo, nami nilikuwa na shughuli nyingi sana nisingeweza kufanya hivyo. Hatimaye, nikapata nafasi ya kukimbia kule, daktari asingeniruhusu kuingia, kasema, "Wewe ni baba, una watoto, wewe, sasa, kamwe huwezi kuingia mle."

103 Nami nikasema, niliona alikuwa Mkatoliki, ndipo nikasema, "Ninataka kukuuliza jambo fulani. Kama ningalikuwa kasisi, na ilinibidi kuingia kumpa taratibu za mwisho, ungeniruhusu?"

Akasema, "Hiyo ni tofauti."

104 Nikasema, "Sivyo kwa watu hawa sivyo. Kwa watu hawa mimi niko tu kadiri kasisi wenu alivyo kwenu." Kisha nikasema, "Ninaenda kumtia mafuta apate kuishi, si kwa ajili ya mauti." Tena nikasema . . .

Akasema, "Vema, anakufa."

Nikasema, "Vema, kama yuafa, basi hivi hutaheshimu imani ya watu hawa?"

105 Naye akanivalisha kama Ku Klux Klan na hatimaye akaniingiza mle. Na kwa hiyo, tukaingia mle ndani, naye maskini nesi mmoja akaja, na—naye akaangalia, naye kwa namna fulani alikerwa na kuingia kwangu kwa vyovyote vile. Kadiogramu, namna fulani ya mtambo pale, tulikuwa tukiuangalia, ulikuwa umeshuka sana, mapigo ya moyo yalikuwa mara *kadhaa* tu.

106 Na kwa hiyo nikamwombea huyo mvulana maneno machache tu ya maombi, nikaweka mikono yangu juu ya jamaa huyo mdogo, alikuwa na umri wa kama miaka kumi na miwili, kumi na minne, nami nikasema, "Baba wa Mbinguni, juu ya msingi wa imani ya maskini baba na mama huyu, wakiniita kumwombea mtoto huyu, na juu ya Neno Lako, Wewe ulisema, 'Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Sasa, wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.'"

107 Nikasema, "Ndiyo kwanza nitoke kwenye mkutano ambako nilikuona Wewe ukifanya ishara kuu na maajabu. Ninaamini kuwa mimi ni mwaminio, kama sivyo nilivyo, saidia kutokuamini kwangu, Ee Mungu." Nikasema, "Kwa ajili ya mtoto huyu, ninaweka mikono yangu juu ya mtoto huyu na kumbariki katika Jina la Yesu Kristo kwa ajili ya uponyaji wake, kwamba atakuwa mzima. Asante, Bwana, kwa kutupa ahadi, ninaiamini." Nikamkabidhi kwa Mungu, nikaondoka.

108 Ndipo maskini yule baba akasimama, na kumkumbatia huyo mama, nao wakakumbatiana, kasema, "Mama, si ni ajabu? Si ni ajabu?" Hakuna hata badiliko moja ndani ya mtoto huyo, angali amelala pale, akimsukumia upumuaji wa bandia akiwa na mtambo wa Pulmotor juu yake. Kasema, "Si ni ajabu? Loo, Mungu ashukuriwe kwa kumponya mwana wetu!"

109 Ndipo maskini nesi huyo akasimama pale na kuangalia, alikuwa ni mtoto tu, mwenye umri wa miaka kama kumi na minane tu, ishirini, maskini Snicklefritz kama ningemwita, mwajua, amesimama pale akitafuna hiyo, akizibua hiyo chingamu, akiangalia huku na huku namna *hiyo*, akasema, "Ulielewa alichosema daktari?"

Ndipo maskini baba huyo akageuka, akasema, "Nilielewa vizuri sana, Mtoto, yale aliyosema." Akasema . . .

Akasema, "Mnawezaje kusimama hapo na kucheka na kupigapigana namna hiyo, wakati mtoto wako, amelala hapa akifa?"

110 Ndipo maskini huyo baba akafuta machozi machoni mwake, na kurudisha hicho kichwa chenye upara nyuma, akamtazama usoni, akasema, "Mtoto wangu, mwanangu hafi, yu hai."

111 Akasema, "Bwana, katika historia yote ya matibabu, wakati hiyo chati," *popote* mkono huo ulipo, "huo ukishuka chini pale, haijawahi kujulikana katika historia yote ya matibabu mkono huo kupata kurudi tena kamwe. Huyu mvulana yuafa, amepoteza fahamu kwa siku mbili. Yuafa."

112 Akaweka mkono wake begani mwake, akasema, "Kipenzi, angalia, umefunzwa kuangalia mtambo huo," kasema, "hilo ndilo unaloangalia, mimi ninaangalia ahadi."

113 Huyo mvulana ameoa na ana watoto wawili sasa. Ni kitu gani? Mnaona? Inategemea kile unachoangalia, usiangalie dalili. Kama ukitimiza yale Mungu aliyosema, uyaamini, hilo latosha. Yeye amefanya hivyo, hilo linalimalizia, yote yamekwisha. Mvulana huyo hakubadilika kwa siku tatu ama nne baadaye, lakini alipona, maana baba na mama huyo wasingekuwa na kitu kingine niani mwao, wasingemruhusu ibilisi aweke takataka zake niani mwao, walidumu moja kwa moja nalo, nao wakalishikilia. Naye anaishi, yeye ni mmishenari huko Afrika, usiku wa leo, akiwa na watoto wawili.

Je, ungetaka kujua huyo alikuwa ni nani? Huyo ni Bob Bosworth, huyo ndiye hasa, mvulana wa mzee Dk. Bosworth. Sasa, haya basi.

114 Sasa, mhubiri huyu, nami daima nimewazia juu ya watu kuwa na dalili, kama mtu yeyote alikuwa na haki ya kuwa na dalili ilikuwa ni Yona. Sasa, yeye alikuwa . . . Kwa hiyo sasa mnataka kuwazia amerudi nyuma: Mikono yake imefungwa nyuma yake, miguu yake imefungwa, yuko katika tumbo la nyangumi, labda mikono arobaini chini ya maji, huku dhoruba ikiwa juu yake. Kila upande alikotazama, ilikuwa ni tumbo la nyangumi, amelala mle kwenye matapiko hayo, akiangalia pande zote, kama aliangalia *huku*, lilikuwa ni tumbo la nyangumi, upande *ule* ilikuwa ni tumbo la nyangumi, kila mahali alipoangalia ilikuwa ni tumbo la nyangumi.

115 Naye alijua ya kwamba alikuwa chini ya bahari. Samaki alikuwa amemmeza, akashuka chini ya bahari, na kulikuwa na dhoruba juu ya hiyo bahari, wakati hata hakuwa salama ndani ya meli kule juu, naye huyu hapa katika tumbo la nyangumi. Sasa, alikuwa na kisa kizuri cha dalili, angalikuwa nacho, lakini mnajua yale aliyosema? "Hizo ni ubatili wa uongo, sitauamini."

Huwezi kumficha mtakatifu kutoka kwenye maombi yake, haidhuru . . . Daudi alisema, "Nikitandika kitanda changu kuzimuni, Yeye atakuwa huko." Hiyo ni kweli.

116 Sasa, aliamini ya kwamba wakati Sulemani alipoliweka wakfu hekalu hilo, na kuomba, na kusema, “Bwana, kama watu Wako wakiwa katika shida mahali popote, na watazame hekalu hili na kuomba, basi sikia kutoka Mbinguni.” Akageuza mgongo wake, mwelekeo bora sana alioweza kupata ni wapi mashariki, kaskazini, magharibi, au kusini, kuelekea hekalu hilo, na kuanza kuomba.

117 Loo, jamani! Naye Mungu, kwa imani ya namna hiyo, sijui alilofanya, ninyi wanasayansi mnaotaka kubishania hilo, sitajua, Yeye angeweza kuweka kihema cha oksijeni huko chini, nijuavyo mimi. Sijui alilofanya, bali alimweka hai siku tatu mchana na usiku.

118 Tena yule mtu aliyeomba maombi hayo, Sulemani, hatimaye alirudi nyuma, nalo hilo hekalu likabomolewa. Na kama Yona, chini ya hali hizo akiwa na dalili za namna hiyo ambazo angeweza kuwa nazo, alikataa kuwa nayo, inatupasaje, usiku wa leo? Huku hatuangalii kuelekea hekalu ambalo mtu fulani aliliweka wakfu, hatuangalii kuelekea kwa mtu aliyerudi nyuma, bali tunaangalia kuelekea Mbinguni, ambako Yesu ameketi mkono wa kuume wa Mungu katika ukuu huko Juu, akiishi daima kufanya maombezi juu ya chochote tunachokiri kwamba Yeye amefanya.

Mungu anaweza kuweka tayari kihema cha oksijeni ama chochote kinachohitajika, Yeye angali ni Yehova-Yire, “Bwana atajipatia Mwenyewe chochote anachohitaji.”

119 Kile . . .? Ndipo tunaona watu kote duniani wakiponywa kila mahali, na kushugulikiwa namna hiyo, na kisha kughadhabika, dalili kidogo, “Kidole changu hakijapata nafuu.” “Tumbo langu bado linauma.” Hiyo inaleta tofauti gani? Usiliangalie tumbo lako, angalia yale Mungu aliyosema. Mungu alitoa ahadi, ni kazi ya Mungu kuishughulikia.

120 Vipi kuhusu Ibrahimu, wakati Mungu alipomwambia atapata mtoto kwa Sara? Alimwoa alipokuwa na umri wa kama miaka kumi na saba, alimshinda umri kwa miaka kumi, walikuwa wameishi pamoja kama mume na mke miaka yao yote, naye Ibrahimu alikuwa na sabini na mitano naye alikuwa na sitini na mitano, wakati Mungu alipotoa hiyo ahadi. Alikuwa amekoma hedhi kwa yapata miaka kumi wakati huo, mabadiliko ya maisha, naye huyo hapo, ndipo Mungu akasema, “Utapata mtoto kwake.”

121 Mbona, ninaweza kumwona Sara akisema, “Vema, mume wangu ni mtu wa Mungu, yeye ni nabii.” Akaanza kutengeneza vijibuti, akiandaa jicho ndege, kila kitu tayari, atampata mtoto huyu.

122 Ungeweza kuwazia mume na mke wakongwe wakienda katikati ya mji sasa, na kusema, “Daktari, tunataka kufanya maandalizi hospitalini. Mimi nina umri wa miaka sabini na

mitano, mke wangu, sitini na mitano"? Mungu. . .Imani ni dhihaka kwa kila kitu ila mtu aliye nayo. Hivyo tu. Lakini yule aliye nayo anajua anachozungumzia, ametiwa nanga.

Baada ya mwezi wa kwanza kupita, unaona, Sara alikuwa amepita wakati huo, "Mpenzi, unajisikiaje?"

"Hakuna tofauti."

"Utukufu kwa Mungu, tutampata kwa vyovyote vile. Mungu alisema hivyo."

Mwaka mmoja ukapita, "Mpenzi, hivi hujajisikia tofauti bado?"

"Hata kidogo."

123 "Haleluya! Utakuwa ni mwujiza mkuu mwaka mmoja kuliko ulivyokuwa kama ingetukia mwaka jana." "Hakusita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini; bali alikuwa na nguvu, akimtukuza Mungu." Hakika.

124 Baada ya miaka ishirini na mitano kupita, sasa mume ana mia moja naye mke tisini, "Unajisikiaje, Mpenzi?"

"Hakuna tofauti, lakini bado nina vijibuti. Tunaingojea. Tutampata kwa vyovyote vile."

125 Kwa nini? Mungu alisema hivyo. Hiyo ni kweli. Hilo latosha. Mungu alisema hivyo. Hilo huondoa kila shauku, kujali, kadhalika. Mnajua litatukia, kwa sababu Mungu alisema hivyo, hilo latosha.

126 Nasi tunapaswa kuwa Uzao wa Ibrahimu. Tukiwa na Roho Mtakatifu, sisi ni Uzao wa Ibrahimu, Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu kupitia ahadi, si kupitia kwa Isaka, wa kawaida, bali kupitia kwa Kristo, wa kimbinguni; ninyi ndugu wahudumu mnajua ninalozungumzia. Lakini alikuwa anaenda kumpata kwa vyovyote vile, akaiamini.

127 Yona aliiamini, haidhuru ilikuwa wapi, hali gani, dalili ngapi, Mungu alitoa ahadi. "Watu Wako wakiwa katika shida" Sulemani aliomba na kusema, "Bwana, kama watu Wako wakiwa katika shida, na watazame mahali hapa patakatifu, basi wasikie."

128 Yona, nabii, alikuwa katika shida katika tumbo la nyangumi, chini ya bahari, naye akageuka kuelekea hekaluni na kuomba, na kukataa kuona tumbo la nyangumi, "Sioni kitu ila lile hekalu, Utukufu wa Shekina, ninaona Nguzo ya Moto ikining'inia juu yake, ninamwona Sulemani, mtiwa mafuta wa Mungu, amesimama pale ameinua mikono yake, akiomba. Mungu, Wewe utanijibu." Akaanza kupumua vizuri, kamba zikatoka mikononi mwake, huenda alisimama, huenda aliketi chini, sijui alifanya nini. Alikaa huko siku tatu mchana na usiku.

129 Na baada ya kitambo kidogo maskini yule nyangumi akazunguka kote kote, kwa safari ya teksi kuzunguka chini

ya bahari. Ndipo baada ya kitambo kidogo, yote...yapata saa nne siku moja, wavuvi wote walikuwa huko nje baharini. Nao walikuwa wamewaomba miungu wakubwa wa baharini asubuhi hiyo, mwajua, wawape siku njema yenye mafanikio, wakiishi katika uzinzi, na chochote kile, wakaingia baharini, nao walikuwa wakivuta nyavu zao.

130 Basi baada ya kitambo kidogo akaja mungu wa baharini, akautoa ulimi wake, naye nabii akatoka moja kwa moja kinywani mwake, akaanza kusema, "Tubuni! Tubuni! Katika muda wa siku arobaini nchi hii itaangamizwa." Mungu anajua jinsi ya kufanya mambo, mungu akamtema huyo nabii. Amina. Akatembea moja kwa moja kupitia Ninawi akisema, "Tubuni!" Naam.

131 Yesu alisema, "Kama vile Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi siku tatu mchana na usiku; ndivyo atakavyokuwa Mwana wa Adamu."

132 Mungu katika nyakati zote ametuma karama, na upambanuzi, na ishara kwa watu. Manabii daima wamekuwa ishara. Kila unapomwona nabii akiinuka, afadhali uwe mwangalifu, Hukumu inakuja. Mwangalie Nuhu, mwangalie Musa, mwangalie Yeremia kabla ya kuingia Babeli, mwangalie Yohana Mbatizaji kabla ya Israeli kukataliwa, na loo, na kadhalika, wakati wote. Manabii ni ishara, nao Wayahudi waliamriwa kuwaamini manabii hawa, na, walipokuja na huu—na ujumbe huu. Mungu, katika nyakati zote...Naye alikuwa akiwaambia watu wa kizazi hiki kiovu kile walichokuwa wamefanya.

133 Basi sikilizeni, kila wakati ambapo Mungu hutuma karama kwa Kanisa, nalo Kanisa linaupokea, ni wakati wa ufanisi sana kwa Kanisa. Lakini wakati Kanisa linapoukataa, ni Hukumu kwa wakati huo.

134 Sasa, ukaja wakati wa Sulemani, ambao Yesu aliurejelea. Sasa, sote tunajua ya kwamba siku za Sulemani zilikuwa—zilikuwa ni wakati wa mafanikio sana kwa Israeli, hakuna vita na mataifa yote yaliwaogopa. Kwa nini? Mungu aliwapa karama, nalo taifa zima likaiamini kwa nia moja. Ulikuwa ni wakati wa mafanikio.

135 Laiti sisi Wamarekani tungefanya hivyo, usiku wa leo, mashindano yote ya makombora, na bomu la atomiki, na vitu hivi vingine vyote vingeweza kuzamishwa katikati ya bahari. Mungu amelipatia taifa hili Karama kuu, Roho Mtakatifu, bali hawamwamini. Hata makasisi, makumi ya maelfu yao, wanamkataa. Makanisa yanamkataa, huku anafanya mambo yale yale aliyofanya wakati wa Pentekoste, na kote katika wakati, mpaka parare wa Kirumi na tunutu wakaula, bali Yeye alisema, "Nitarudisha tena, asema Bwana." Atafanya hivyo.

136 Sasa, angalieni, Sulemani katika siku zake, jinsi hilo lilivyo kuu. . . alikuwa na karama ya upambanuzi, ndipo watu wote wakaunganika kwenye karama hiyo, hakuna mtu aliyeipinga.

137 Vipi kama ilikuwa, leo, kwamba kila mtu, hata watu wa Full Gospel, wangezungumza tu kwa utukufu sana, dhidi ya. . . kuhusu Roho Mtakatifu? "Ni ajabu jinsi gani kwa kila mtu!" Vipi kama kila mtu Marekani aliyedai kuwa Mkristo angeiunga tu mkono Karama ya Roho Mtakatifu? Loo, jamani! Ule Utawala wa Miaka Elfu ungekuwa ukiendelea, hakika ungeendelea. Lakini tofauti zetu ndogondogo kati ya nyua zetu za kimadhehebu, na kadhalika, zimewatenganisha kama mashariki ilivyo mbali na magharibi. Wala Mungu kamwe hataweza kutufanyia lolote mpaka hizo kuta zitakapobomolewa, nasi tunakuwa mmoja katika Kristo. Hiyo ni kweli.

138 Tunawaona pale, na hao hapo, wote, kila mahali ungeenda, useme, "Loo, si ilikuwa ni ajabu? Wananiambia ya kwamba Mungu alimshukia Sulemani jana na jambo kuu likatukia. Loo, utukufu kwa Mungu!" Mtu mwingine akamwambia mtu mwingine, na mtu mwingine, "Loo, haleluya kwa Mungu!" Ulikuwa ni wakati wa upeo wa mafanikio.

139 Vipi kama Kanisa lingekuwa namna hiyo siku hizi, ndugu? Si lingekuwa ni jambo zuri sana? Ninii tu, loo, tungefanya nini? Si lingekuwa ni jambo zuri sana? Hakungekuwa na. . . Hakuna kitu kingeninii. . .

140 Kweli tungekuwa na kimbilio la bomu, lisingechimbiwa chini ardhini. Hayo mabomu yatalipua shimo chini ardhini umbali wa yadi mia moja na hamsini, ama yadi mia mbili, ama kitu kama hicho, ndani kabisa ardhini, na kuenea kwa maili mia moja na hamsini. Mbona, kama ungekuwa ninii elfu. . . kama ungekuwa huko chini kwenye lava, ingevunja kila mfupa mwilini mwako.

141 Huwezi kuchimba chini, inakubidi kuchimba juu uiondokee. Tunalo kimbilio, nalo limetengenezwa kwa manyoya: chini ya mbawa Zake. Amina. Tutachukuliwa. Loo, nina furaha sana kwa ajili ya kimbilio hilo! Naam, bwana. Chini ya mbawa Zake. Mbona, mavumbi hayatatulia mpaka tutakapokuwa Utukufuni. Hiyo ni kweli. Salama chini ya mbawa Zake. Loo, jinsi mbawa kubwa za Tai zitakavyotubeba kutoka hapa moja ya siku hizi!

142 Sasa, ndipo tunaona, basi, ya kwamba katika wakati huu mkuu, Mungu akitenda kazi, hilo taifa zima likistawi likawa kitu kimoja kikuu, kitukufu. Mbona, mwajua, haikukaa tu katika taifa hilo, bali ilienda kwa mataifa mengine, taifa baada ya taifa!

143 Hawakuwa na televisheni wakati huo, wangeuchafua ulimwengu kama vile wamefanya nayo sasa. Kila mtu akikaa nyumbani Jumatano usiku kuangalia *Tunampenda Susie*, ama kitu fulani cha kijinga kama hicho. Wakristo! Tsk, tsk, tsk, tsk, tsk, tsk! Hiyo inaonyesha ni roho ya namna gani iliyo

ndani ya watu, wanapopenda upuuzi mtupu wa namna hiyo wa Hollywood, kinyaa na uchafu, wamefunga ndoa mara kadhaa, wakiishi huko nje kama mbwa, halafu wanakuja na . . . Upuuzi huu! Halafu watu wanakaa nyumbani mbali na mkutano wa maombi. Inaonyesha mahali mioyo yao ilipo, hiyo ndiyo sababu hakuwezi kuwa na u—uamsho. Hiyo ni kweli.

144 Hata hivyo, hapo ndipo mahali pa mchungaji wenu, mnaona, yeye anawaambia jambo hilo. Sikilizeni, ninawaambia tu pia, ili mpate kujua sehemu yangu, aminini hilo, pia, ninaliamini jambo lilo hilo. Naam, bwana. Ee Mungu! Tunachohitaji ni uamsho kote kutoka mimbarani hadi kwa bawabu, uchocheeni, u—uamsho wa Kipentekoste wa mtindo wa kale, wa nyuma msituni, anga-bluu, uliotumwa na Mungu. Hiyo ni kweli. Si kupakwa chokaa, bali kuoshwa ukawa mweupe. Hiyo ni kweli. Si kusema, kuzungumza juu ya utukufu wa Mungu, bali Mungu wa Utukufu akifunua utukufu wa Mungu. Hilo—hilo ndilo tunalohitaji Ka—Kanisani siku hizi.

145 Angalieni, wakati ule mkuu wa Sulemani, jinsi ulivyoendelea, jinsi ulivyokuwa tukufu! Watu wengine wakaanza kuwaambia wengine, nao wakati huo walisafiri kwa msafara, na kwa hiyo wakapitia kwenye kundi la ngamia wakienda katika nchi nyingine, nao wangeshuka waende katika nchi nyingine na kusema, "Aisee, nakwambia, Israeli hiyo, hujawahi kuona kitu kama hicho maishani mwako! Wana uamsho unaoendelea kule juu, Mungu wa Utukufu yuko miongoni mwao. Nao wamemchukua mtu huyo mwenye karama hiyo kuu na kumfanya mfalme wao. Naye Mungu anaheshimu kila kila afanyacho, kikamilifu kabisa."

146 Mnajua, hatimaye ilifika moja kwa moja hata pande za mwisho za dunia, hadi Sheba, hiyo ni huko chini kabisa, mbali kabisa chini ya jangwa la Sahara, na kulikuwako na maskini malkia kule chini. Mwajua, mtu fulani alipitia na kumwambia habari zake, naye kamwe asingeweza tu kungojea mpaka msafara mwingine uje.

"Ulisikia . . .?"

"Je, ulipitia Palestina?"

"Naam."

"Ndivyo ilivyo?"

"Loo, ni ninii tu, nilienda na kuiona, ni ya ajabu sana!"

147 "Imani chanzo chake ni kusikia Neno la Mungu." Maskini moyo wake ukaanza kuona njaa. Mnaona? Ilikuwa ni kitu gani? Hiyo Nuru ilimulika juu ya Mbegu hiyo, ingawa hakuwa Myahudi, alikuwa kafiri, bali alikuwa amekusudiwa Uzima wa Milele. Aliisikia, huenda wengine waliisikia na hawakuijali, "Loo, upuuzi, kundi la watakatifu wanaojibingirisha." Lakini

aliiamini, kulikuwa na kitu Fulani ndani yake, kilichosema, “Hiyo inasikika nzuri sana.”

Wakati mwingine msafara mwingine ukapitia, “Mlipitia Palestina? Niambieni.”

148 “Loo, ngoja, ninajua kile utakachoniuliza. Hao watu wana moyo mmoja na nia moja, taifa zima, naye Mungu anatenda kazi pamoja nao. Wana mtu huko juu aliye na karama ya upambanuzi. Hujawahi kuona kitu kama hicho, Mungu akitenda kazi pamoja nao.”

Hakujua upambanuzi ulikuwa ni nini, alikuwa ni mpagani, “Unamaanisha nini na hilo?”

149 “Inamaanisha ya kwamba Mungu wa hekima yote anamshukia mwanadamu na kumfunulia siri za watu.” Loo, hilo lilikuwa ni jambo zuri jinsi gani! Moyo wake ukaanza kuona njaa.

150 Sasa, alikuwa na upinzani mwingi, hakika alikuwa nao, bali imani yake haikuwa na wowote. Mwajua, imani haina upinzani. La. Huenda ukawa na mwingi sana, lakini imani yako haina, kama ni imani ya kweli ya kuzaliwa mara ya pili. Imani yake haikuwa na upinzani.

151 Sasa, yeye alikuwa mpagani. Hebu tufanye mchezo mdogo wa kuigiza hapa kusudi watoto walipate. Kesho yake asubuhi ninamwona akiamka, na kuoga, na kujiandaa, nao maskini wajakazi wake wakamtayarisha, kumbukeni, yeye ni malkia. Kisha anaondoka kwenda hekaluni kukariri sala zake za asubuhi, na, loo, kila kitu kilichombidi kufanya, mwajua, na kukutana na baba mtakatifu, na hao wote, labda abusu pete zake na miguu yake, na kadhalika, na kutekeleza dini yake yote.

152 Basi wakati akisimama pale, alisema, “Baba Mtakatifu, ninataka ku—kukwambia jambo fulani. Nasikia ya kwamba huko Palestina, wana Mungu huko juu anayeishi ndani ya mwanadamu, akijionyesha Mwenyewe kupitia mwanadamu.”

153 “Hmm, binti yangu,” huo hapo upinzani wako, “sasa, huo ni upuuzi tu. Watu hao daima ni watu wa namna hiyo, daima jambo fulani linaendelea, kwa kweli ni bure, kuhusu kuvuka Bahari ya Shamu, na mambo hayo yote ya kila namna, ni bure kabisa, ewe mtoto. Kama kungekuwa na jambo lolote linaloendelea namna hiyo, mungu wako mwenyewe hapa angekuwa akilifanya, lingekuwa juu ya kuhani wako mwenyewe.” Lakini mnaona, Mungu ana njia za kufanya mambo. “Lingekuwa papa hapa kwenye dhehebu lako mwenyewe. Kama jambo lolote lingetukia namna hiyo, lingekuwa papa hapa.”

154 Ninaweza kumsikia maskini malkia huyo, huenda alikuwa na jibu zuri kwake, huenda alisema, “Sasa, sikiliza, mama yangu alihudumu katika hekalu hili, alisoma vitabu vyenu vyote, alinifundisha hivyo vitabu vyote, mama yake alimfundisha

vitabu vyote, mama yake alimfundisha vyote, kizazi baada ya kizazi. Tumeona michongo, na sanamu, na kusikia hadithi, bali hatujaona msogeo mmoja wa chochote bado. Nao wananiambia ya kwamba kuna Kitu fulani huko juu ambacho ni halisi. Kuna Kitu fulani, kilicho halisi, unaweza kukiona kwa macho yako na kukiona kikitenda kazi kwa mtu aitwaye Sulemani."

155 "Sasa, angalia hapa, Binti, wewe ni malkia, usingechanganyikana na kundi la watu kama hao. Usingefanya hivyo, kamwe usingeweza kushusha heshima yako."

156 "Iwe hadhi isiwe hadhi, Kitu fulani kinaniambia kwamba lazima niende. Mtu fulani aliniletea Gombo, nami nikasoma ya kwamba hivyo ndivyo Mungu wao alivyo, Yehova, Naye *anatenda* Mwenyewe ndani ya mtu huyo. Sasa, sijaona moja ya sanamu hizo ikisogea bado, lakini tunamwona katika mwanadamu."

157 "Ah, upuuzi! Sasa, angalia, Binti, ukifanya hivyo, ingawa wewe ni malkia, mimi ni kuhani mkuu, itanibidi kukutenga na imani hii ya kifalme ambayo nyanya wa nyanya yako, -mama, -mama, -mama, na kadhalika, wote walitumika katika hekalu hili."

"Vema, afadhali uondoe jina langu kwenye hicho kitabu sasa hivi, kwa sababu ninaenda."

Mwajua, kuna jambo fulani kulihusu, Mungu anapoushika moyo wa mwanadamu, hakuna kitu kitakachowazuia. Hiyo ni kweli.

158 Sasa, anarudi, alikuwa na upinzani mwingi, ilimbidi kwanza kuliacha kanisa lake, ndipo akasema, "Sasa, hebu niwazie, kama hiyo ni kweli, sasa, ninachukua tu neno la mtu mwingine, kama hiyo ni kweli, nitapeleka pesa huko juu na kuiunga mkono, lakini kama si ya kweli, nitazirudisha."

159 Sasa, hilo lingefaa kwa Wapentekoste kusikia baadhi ya hayo. Mnaunga mkono vipindi vya redio vinavyowadhihaki, hiyo ni kweli, vipindi vya redio vinavyowadhihaki, na wanaume wenu wenyewe wakiomba pesa, hiyo ni kweli, kuunga mkono mradi wake mwenyewe. Hiyo ni kweli.

160 Kama ni wa Mungu, dumu nao, kama si wa Mungu, uondokee. ". . . Mungu akiwa ni Mungu, mtumikieni," alisema Eliya, "kama Yeye si Mungu, basi tafuteni kujua Mungu ni Nani kisha mkamtumikie."

161 Aliwapakia ngamia vifurushi vikubwa vilivyojaa almasi, na uvumba, na manemane, na kadhalika, naye akawapakia kabisa. Sasa, alikuwa na falsafa nzuri, "Kama ni ya Mungu . . . Ninasoma Vitabu kuhusu Mungu ni nani, na kama nikimwona Yeye *akitenda* Mwenyewe ndani ya mtu huyo, ninajua Yeye ni Mungu anayewajali watu Wake, na kuishi ndani ya watu Wake. Nami ninaenda kutafuta kujua."

162 Sasa, kumbukeni, alikuwa na safari ndefu. Inachukua siku tisini, miezi mitatu, juu ya mgongo wa ngamia kupitia jangwa lenye joto la Sahara, juu ya mgongo wa ngamia, si Kadilaki iliyoyoyozwa, sasa, juu ya mgongo wa ngamia, kuja kutoka Sheba kwenda Yerusalemu. Wazia, siku tisini! Si ajabu Yesu alisema atasimama katika siku za mwisho na kukihukumu kizazi hiki. Alikuja umbali huo wote, na kujitolea huko kwote akaisikie hekima ya Sulemani, nao watu hawatavuka barabara, papa hapa, katika Santa Maria. Angalia kile alichofanya. Mbona, Nuru ilikuwa imemulika juu ya Mbegu hiyo, ikawa Hai! Haijalishi kile . . .

163 Sikilizeni, hili hapa jambo lingine: Kumbukeni, watoto wa Esau walikuwa jangwani siku hizo, nao walikuwa ni wapanda farasi hodari sana, na wanyang'anyi. Ingekuwa ni rahisi jinsi gani, hilo kundi dogo la walinzi alilokuwa nalo, kukatwakatwa kisha wachukue hazina hiyo yote!

164 Lakini mnaona, imani haioni upinzani wowote. Sijali kama mume analipinga, mke analipinga, kama *huyu* analipinga, na *yule* analipinga, kama kweli una imani kwa ajili ya uponyaji wako, utalishikilia, sijali, hata daktari akisema sivyo, utaamini kwa vyovyote vile. Haijui upinzani wowote, inadumu moja kwa moja nalo.

165 Ana kundi la maskini matowashi, mlinzi wake, na wajakazi wachache, juu ya ngamia, labda walisafiri usiku, kulikuwa na joto sana jangwani, na kupumzika kwenye oasisi mchana kutwa, naye alikuwa akisoma Magombo haya, yale ambayo Yehova alikuwa ameahidi. Alitaka kuhakikisha ya kwamba alisoma Neno na kuona ya kwamba karama hii ililingana na Neno.

Hilo hapo jambo la kufanya, lichunguze. Chunguza mambo haya yanayoendelea huku siku hizi, uone kama ni ya Bwana, yachunguze kwa Neno.

166 Mnajua, Mungu alikuwa na njia ya kufanya mambo katika Agano la Kale. Kama ndivyo, nabii alitabiri, naye akashuka akaenda kwenye Urimu na Thumimu, kile kifuko cha kifuani kilichotundikwa hekaluni, ndipo basi, walipotabiri, na kama Urimu na Thumimu, Nuru za kimbinguni zilimulika juu ya hiyo, nabii alikuwa akisema kweli, kama hazikumulika, haidhuru inasikika halisi jinsi gani, ilikuwa ni uongo, ama mwotaji, ama chochote kile, ilikuwa ni makosa kama Urimu na Thumimu haikuonyesha kwamba ni kweli. Sasa, ukuhani wa Haruni, ulipokoma, Urimu na Thumimu ilienda pamoja nao, kile kifuko cha kifuani.

167 Lakini Mungu ana Urimu na Thumimu nyingine, hiyo ni Biblia. Hebu imulike katika Biblia, na hebu hizo Nuru ziangazie . . . Nuru zimulike katika Biblia. Useme, "Mungu aliahidi jambo hilo, nalo hili *hapa*. Ni ahadi." Ndipo unajua uko sahihi. Mungu na Urimu na Thumimu Yake! "Wasiponena

sawasawa na torati na manabii, hamna Nuru ndani yao." Sasa, hebu hiyo iwe ndiyo Nu—Nuru.

168 Alikuwa anaenda kuchunguza. Aliisoma, mchana kutwa aliketi chini ya miti na kusoma haya Magombo ya manabii mbalimbali. Naye alikuwa akiangalia aone kitakachotukia atakapofika kule. Hatimaye akawasili, akawasili nyuani.

169 Sasa, watu wengi, wakati uamsho unapokuja mjini ukizungumza juu ya Mungu, uamsho wa Kipentekoste, baadhi yao husema, "Vema, ninaamini nitaenda kule, nikawasikilize hao watakatifu wanaojifingirisha, usiku wa leo." Yeye ataninii . . . Wataenda kule na kuketi chini, na jambo la kwanza linalosemwa ambalo linapingana na maskini fundisho lao duni, liwe la Kimaandiko ama sivyo, hao wanatoka nje ya jengo, hivyo tu.

170 Yeye hakuja afanye hivyo, aliwafungua tu ngamia wake na kupiga mahema, naye alikuwa akae huko mpaka atakaposhawishika. Hilo ni wazo zuri, napenda hilo. Alikuwa na Magombo yote, angeweza kuyasoma na kuona kama ni kweli ama si kweli, angeyalinganisha na Neno ambalo huyu Mungu alikuwa amenena habari zake. Kwamba . . . Alikuwa mwanamke mwerevu, hakika alikuwa.

171 Tunawahitaji wengi zaidi siku hizi. Halafu . . . Wangekuwa wanawake waliovalia vizuri zaidi, wenye nywele ndefu, wakiachana na kaptura na kadhalika, kama wanavyopaswa kufanya. Badala ya kuwafuatisha wengine, huku chini Hollywood, wangekuwa wakiiga mfano wa Mungu hapa katika Biblia. Hiyo ni kweli.

172 Ndipo wa kwanza . . . Kumbuka, dada, wakati nikiwa kwenye hili somo, mwanamke anayevaa kama mmojawapo wa hawa wanyama waliochunwa ngozi walio hapa nje mtaani, akitembea mtaani, hivi mnajua Yesu alisema, "Kila amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye moyoni mwake?"

173 Unasema, "Mimi ni safi tu kama yungiyungi." Huenda ukawa kwa mumeo au mvulana mpenzi wako, lakini ukivalia hivyo, naye mwenye dhambi akuangalie namna hiyo, naye awajibike kwa ajili yake kwenye Siku ya Hukumu, alizini na nani? Wewe. Ni kosa la nani? Lako, kwa kuwa ulijianika mwenyewe. Hiyo ni kweli.

"Loo," unasema, "hiyo ndiyo aina pekee ya nguo wanazotengeneza."

174 Wangali wanatengeneza cherehani na kuuza vitambaa, hakuna udhuru. Kwa sababu maskini roho hiyo ya tamaa mbaya ilikuja juu ya wanawake, ikiwaingiza wanawake wengi safi katika upuuzi mtupu na . . . Hilo ni Neno la Bwana. Hatuna budi kurudisha tena ile imani halisi waliyokabidhiwa mara moja tu hapo mwanzo. Makanisa yetu ya Kipentekoste, mchwa

wamekula msingi kutoka chini yake kwa upuuzi kama huo, hakika. Biblia ilisema hivyo, ni aibu na fedheha. Ilikuwa kwamba, ilikuwa ni vibaya kwao kufanya hivyo, lakini sasa wameachilia mambo.

Ma—maskini mhudumu wa Kimethodisti alikuwa akiimba wimbo, akasema:

> Tulilegeza kamba, Tulilegeza kamba,
> Tukapatana na dhambi.
> Tulilegeza kamba, kondoo wakatoka nje.
> Lakini mbuzi waliingiaje?

175 Mlilegeza kamba, hivyo ndivyo ilivyokuwa. Mkarudia namna fulani ya fundisho la sharti, kisha wanapiga kelele kuhusu kanisa la Kirumi na fundisho lao la sharti, nasi tunalo papa hapa kwenye mlango wetu wa nyuma. Chungu hakiwezi kusema birika ni chafu. La, bwana. Hiyo ni hakika. Hiyo hapo Biblia moja kwa moja mbele zetu. Ni—ni chukizo.

176 Mwanamke fulani aliniambia, kasema, "Mimi sivai kaptura, mimi huvaa hizi. . ." Aliziitaje? Wanapozivuta juu kama. . .? "Suruali ndefu."

Nikasema, "Hizo ni mbaya zaidi kuliko hapo awali. Biblia ilisema ni chukizo kwa mwanamke kuvaa vazi limpasalo mwanamume." Ni aibu.

177 Loo, wanawake wetu, wanaume wetu! Nanyi wanaume mlio na mfupa wa shingo ya kuku badala ya uti wa mgongo, kuwaacha wanawake wenu wavute sigara, na kutenda hivyo, aibu kwenu! Simwiti huyo mtawala wa nyumba yake mwenyewe, namwita huyo mtu anayeongozwa kwa masikio mahali fulani. Aibu kwenu. Loo, "Mwili we—wetu wote," Isaya alisema, "umekuwa vidonda vitokavyo usaha." Tunahitaji kusafishwa kwa nyumba na uamsho wa Roho Mtakatifu, kwa ajili ya Kuja kwa Bwana Yesu Kristo, kusafishwa kutoka mimbarani. . .Hiyo ni kweli. Mnajua hiyo ni kweli.

178 Sasa, haya twende. Maskini malkia huyo alitoa mabunda yake, na kuyaweka chini, akapiga mahema yake, naye alikuwa akae mpaka aliposhawishika. Ninaweza kumwona akija asubuhi ya kwanza, tarumbeta zikipigwa, na vinanda vikapigwa, na muziki wote ukapigwa, na vinanda na kadhalika. Nao wakawa na mkutano mkubwa sana asubuhi hiyo, wakafurahi katika Bwana, na kumsifu Bwana huku tarumbeta elfu moja zikipiga kelele za utukufu Wake. Ndipo dhabihu ikatolewa, moshi ukapanda juu, nao watu wakaanguka kifudifudi na kuabudu. Yote yalikuwa mapya kwake.

179 Ndipo baada ya kitambo kidogo, Mchungaji Sulemani akatokea akitembea. Loo, jinsi kila mtu alivyompenda! Jamani, si lingekuwa ni jambo zuri sana kama watu wetu wangempenda Roho Mtakatifu anaposhuka namna hiyo? Tunatii tu, na kuwa wanyenyekevu sana Kwake.

180 Mchungaji Sulemani alitoka nje kwa heshima sana, akainama mbele ya watu. Na ninii . . . Vema, angali ni mfalme, lakini katika unyenyekevu wake, mzuri na mnyenyekevu, hakuomba mambo makuu, apate tu hekima ya kuwaongoza watu wake.

181 Ndipo akaanza kuona mstari wa maombi, tuseme, asubuhi hiyo, kwamba siri za mioyo ya watu zilikuwa zikifunuliwa. Ninawazia alikesha usiku kucha akisoma hayo Magombo, "Niliiona kwa macho yangu mwenyewe. Niliiona kwa macho yangu mwenyewe. Niliiangalia."

182 Hatimaye namba yake ikaitwa, wakati wake ukafika. Akaja mbele ya Sulemani, nayo Biblia ilisema hakuna hata jambo moja ambalo Mungu hakumjulisha. Loo, jamani! Moyo wake ha-. . . Alisisimkwa sana, akageuka na kumbariki Mungu wa Sulemani, na akawabariki watu walioandamana naye, akasema, "Heri ninyi mnaokaa hapa, na macho yenu yanauona utukufu huu siku baada ya siku." Amina. Amina. Si ajabu Yesu alisema atasimama katika Siku ya Hukumu na kukihukumu kizazi hicho, kwa sababu hapo alikuwapo aliye mkuu kuliko Sulemani. Hiyo ni kweli.

183 Ndugu, dada, ilikuwaje? Aliona kitu halisi kwa mara yake ya kwanza maishani. Tunapaswa tu kuwa na muda zaidi, bali tunapaswa kuwa tunafunga sasa hivi. Aliona kitu halisi kwa mara yake ya kwanza, kilikuwa ni kitu halisi, kitu ambacho hakikuwa cha kujifanya. Aliona kitu kilichotoka kwa Mungu, kwamba mwanadamu asingeweza kuwa na hekima hiyo mwenyewe. Angezijua siri na kuzifunua, karama, alikuwa ni nabii, naye—naye angeweza kuelewa na kujua ninii . . .

184 Na hapa Yesu, Mwana wa Mungu aliyetiwa mafuta, akisimama pale, alikuwa mkuu kuliko Sulemani, nao wakaiita roho ya ibilisi, "Yeye ni mpiga ramli."

Akasema, "Malkia huyo atasimama Hukumuni pamoja na watu wa kizazi hiki, na kuwahukumu kuwa wamekosa."

185 Sasa, kama akiinuka na kuwahukumu watu wa kizazi *hicho*, ni zaidi sana vipi atakihukumu kizazi *hiki*? Baada ya miaka elfu mbili ya Injili, na jasho na kazi ngumu, na Roho Mtakatifu akitenda kazi makanisani na kulithibitisha, kukiweko na Biblia iliyochapishwa na kila kitu kimewekwa mbele zetu, nasi tunaona kazi Zake zikiendelea, na hata hivyo tunasimama kana kwamba tulikuwa ni lundo la nyasi kavu mahali fulani. Ati nini? Maskini huyo malkia, nitafunga kwa kusema hivi, aliona kitu ambacho kilikuwa halisi.

186 Sasa, sikilizeni, kabla tu hatujaanza, na kuitisha mstari wa maombi, ningetaka kusema jambo hili, napenda kuwinda kama mjuavyo, niliwaambia kuhusu ile bunduki, hadithi ndogo inakuja niani mwangu ninayotaka kuwasimulia, kabla tu ya kufunga.

187 Nilikuwa, kabla sijaingia katika kazi ya uinjilisti, nilikuwa . . . nilikuwa na kopo la hamira, nilihifadhi hela na kadhalika, wakati ni—nilipokuwa mlinzi wa wanyama. Nilifanya kazi na nikachunga kanisa la Baptisti, Maskani ya Baptisti huko Jeffersonville, kwa miaka kumi na saba bila hata senti moja ya mshahara, sikuchukua mshahara, kamwe sikuchukua sadaka maishani mwangu. Kwa hiyo ningeingiza hela zangu, nilipolipwa, mle ndani ili kufanya ziara ya mawindoni mara moja kwa mwaka.

188 Nami nilikuwa nikiwinda kwenye misitu ya kaskazini pamoja na marafiki fulani huko juu. Na mwindaji hodari, jamaa niliyewinda naye, jina lake lilikuwa Call, Bert Call, jamaa mzuri, karibu nusu-Mhindi pia. Na yeye—yeye alikuwa ni mwindaji mzuri, nilipenda kuwinda pamoja naye kwa sababu haikukubidi kumtafuta, alijua mahali alipokuwa. Na mwenye shabaha? Jamani, alikuwa mwenye shabaha sana! Lakini mtu katili kuliko wote niliyepata kukutana naye maishani mwangu. Mtu huyo kweli alikuwa katili. Alikuwa na macho kama ya mjusi, nayo yamekaa kombo, mwajua, namna hiyo.

189 Naye alikuwa akiwapiga risasi maskini watoto wa kulungu ili tu kunifanya nijisikie vibaya. Naye angepiga risasi ninii . . . Mnajua mtoto wa kulungu ni nini, ni mtoto mdogo mchanga wa kulungu. Naye angewapiga risasi kulungu jike, mama kulungu na watoto wa kulungu, na kadhalika. Sasa, ni sawa, kama sheria . . . Sasa, mimi sininii, ninyi ndugu wawindaji, sishutumu kumwua mtoto wa kulungu, hilo ni sawa, kama sheria inasema umwue. Lakini kuwapiga risasi tu kwa kujifurahisha, hilo ni kosa, hayo ni mauaji. Katika kitabu changu ni mauaji, hiyo ni kweli, kuwaua tu ili kuua.

190 Sasa, si kwa sababu alikuwa ni mtoto wa kulungu, sasa, Ibrahimu alimchinja ndama, naye Mungu akamla. Kwa hiyo hapo, si jinsia, ama ninii—ama ukubwa, bali ni kuwaua tu kikatili, kuua. Na hivyo ndivyo Bert angefanya, ku—kuwa tu katili, kupata . . . kunifanya nijisikie vibaya. Angewapiga risasi hao jamaa wadogo na kuwaangalia wakianguka huko, kwa kujifurahisha tu.

191 Nami . . . Mwaka mmoja nilipanda huko juu, kidogo ilikuwa imechelewa, nami nikapanda juu. Naye Bert, tulikuwa . . . alikuwa akiningojea kwa siku mbili. Nilikuwa . . . Niliwaambia nilichelewa sikuzote, na hata kwenye safari zangu za kuwinda. Kwa hiyo yeye . . . Nilichelewa.

Akasema, "Umekuwa wapi, Mhubiri?"

Nikasema, "Kamwe nisingeweza kutoka kazini, Bert." Tulikuwa moja kwa moja katika msimu wa kware. Nikasema, "Nisingeweza kutoka kazini."

192 Akasema, "Vema, itachelewa." Kasema, "Nimekuwa nikiwinda hapa juu sasa kwa siku kadhaa." Kasema, "Maskini

hao mikia myeupe ni kama Houdini, yule bingwa wa kutoroka. Wametoroka katika sekunde moja." Naye akasema . . .

Nikasema, "Vema, tutajaribu, tunajua mahali tulipo. Tuna yapata siku kumi sasa, tutapata mmoja."

Kwa hiyo tukaanza safari asubuhi hiyo, naye akasema, "Ninataka kukuonyesha kitu fulani, Mhubiri. Hujawahi kuona kitu kama hicho."

Nikasema, "Ni kitu gani, Bert?"

193 Akaingiza mkono mfukoni mwake, akatoa filimbi ndogo, akaipiga, akaipulizia, nayo ikasikika tu kama mtoto mchanga wa kulungu, akimlilia mama yake.

Ndipo nikasema, "Sasa, Bert, usingekuwa katili hivyo."

Naye akasema, "Loo, wewe ni kama wahubiri wengine wote; wewe ni mwoga sana huwezi kuwa mwindaji." Akasema, "Jirudie, ewe Jamaa."

Nikasema, "Bert, huko—huko si kuwa mwoga, huko ni—huko ni kutenda ukitumia akili." Nikasema, "Usifanye jambo kama hilo, Bert."

Akasema, "Aa, endelea, Billy. Kwani una shida gani?"

194 Kwa hiyo sikuzote sisi hubeba chokoleti, chokoleti ni bora kuliko kahawa, maana inachangamsha. Wakati mwingine unazungushwa mwituni, na huenda ikakubidi kukaa nje usiku kucha, na afadhali uchukue chokoleti kidogo, ama chochote kile, kukudumisha joto usiku kucha, kama huwezi kupata kitu kikavu cha kuwasha moto.

195 Kwa hiyo tuliwinda mpaka yapata, yapata saa tano, wala hatukuona mburuzo wala ishara, yapata inchi nne, inchi sita za theluji, hali ya hewa nzuri ya kufuatilia, hakuna hata ishara popote, usiku wa mbalamwezi, bila shaka na hao kulungu wakila usiku, bali tusingeweza kupata hata mburuzo, nami nikasema, "Vema, itakuwa mbaya sana."

196 Tukazidi kwenda mbele, yapata saa tano, na kwa ghafla, yeye kwa namna fulani . . . Akafika mahali pa wazi, pana yapata ukubwa wa karibu mara mbili ya jengo hili hapa, Bert kidogo akainama chini, naye akarudisha mkono wake kwenye koti lake namna *hii*, nami nikawazia "Vema, anaenda kuninii . . . tunaenda kula chakula cha mchana, na labda tutengane, ndipo aende njia moja nami nyingine, tuingie ndani kabisa. Saa tatu ama saa nne, usiku wa leo, tutarudi kwenye kambi yetu."

197 Kwa hiyo akanyosha mkono pale, akatoa filimbi hii ndogo, nami nikasema, "Sasa . . . " Nilifikiri alikuwa akitaka kutoa chakula chake cha mchana, lakini alitoa hii filimbi ndogo, na akaiweka kinywani mwake, na kutoa mwito mdogo kama mtoto mchanga wa kulungu anayemlilia mama yake, mwajua, namna hiyo. Basi alipofanya hivyo, aliniangalia.

198 Nami nikaona moja kwa moja kwenye uwazi mdogo pale, kulungu jike mkubwa mno, wa kupendeza alisimama. Mnaona? Alikuwa amejificha, lakini aliposikia wito huo wa mtoto huyo mchanga, yeye alikuwa ni mama, silika iliyo ndani yake ikapanda. Sasa, asingefanya hivyo kwa kawaida, wakati huo wa mchana. Lakini ningeweza kuona hayo masikio makubwa namna *hiyo*, na hayo macho makubwa ya hudhurungi yakiangalia kila mahali. Ilikuwa ni kitu gani? Mtoto mchanga na mama. Ndipo akaniangalia, na hayo macho ya mjusi yakaniangalia.

Nikawaza, "Bert, hungefanya hivyo. Hungefanya hivyo."

199 Akasema, "Shh," kisha akaichukua hiyo filimbi tena, akaipuliza tena, naye huyo kulungu akaingia moja kwa moja kwenye uwazi huo. Loo, jamani, hilo si la kawaida! Nami nikamwona akiangalia juu tena, akauvuta nyuma ule wenzo, kisha akatupa hiyo risasi kubwa ya mia na themanini katika hiyo .30-06, alikuwa mlenga shabaha hodari.

200 Nilimwona akilenga chini namna *hii*, mwajua, nami nikawazia, "Loo-lo. Sekunde moja tu zaidi, naye atausukuma moyo wa mama huyo, moyo huo mwaminifu, moja kwa moja kupitia kwake" mnaona, "huku risasi hiyo kubwa ya uyoga ukubwa wa themanini ikipita moja kwa moja kwenye moyo huo mwaminifu. Mama akimtafuta mtoto wake mchanga! Ungewezaje kuwa mdanganyifu hivyo?"

201 Akakanyaga-kanyaga wakati ko—komeo lilipofungwa kwenye bunduki. Mnajua ni kitu gani, katika muundo 70, komeo linapofungwa, linatoa sauti kidogo. Akageuka, akamwona huyo mwindaji. Sasa, kwa kawaida yeye hutoweka, tunavyosema, [Ndugu Branham anadata vidole vyake—Mh.] ameenda, namna *hiyo*, bali si yeye. Alikuwa moja kwa moja mbele ya mauti, bali mtoto wake mchanga alikuwa na hitaji, yeye alikuwa mwaminifu. Hakuwa mnafiki, hakuwa akiiga kitu fulani, hakuwa wa kujifanya mwaminio, alikuwa ni mama. Kulikuwa na kitu ndani yake, alikuwa mama.

202 Ndipo nikawazia, "Ee Mungu, hilo hapo somo! 'Hata hivyo mama anaweza kumsahau mtoto wake anayenyonya, lakini kamwe sitakusahau. Jina lako limechorwa katika vitanga vya mkono Wangu.'"

203 Nikawaza, "Bert, hakika huwezi kufanya hivyo." Nilikuwa nyuma ya kichaka karibu na huyo kulungu, lakini nilikuwa nikiangalia kupitia—kupitia kwenye baadhi ya theluji kwenye msonobari mdogo na kuangalia, naye. . . Nikaona hiyo bunduki ikiinuliwa pale. Na loo, jamani, alikuwa jinsi—jinsi alivyokuwa mlenga shabaha hodari!

204 Nisingeweza kuliangalia. Nikawaza, "Huyo mama mwaminifu," nikawaza, "jinsi alivyo halisi! Amejitokeza moja kwa moja huko nje mbele ya mauti." Na hayo masikio,

hiyo pua, akamwona huyo mwindaji ameketi pale, lakini hilo halikuleta tofauti, alikuwa tayari kuingia mautini. Kwa nini? Mtoto huyo alikuwa akilia, naye alikuwa akijaribu kumtafuta, alikuwa ni mama. Kulikuwa na kitu ndani yake, kilichokuwa ni mama, ndani yake. Alizaliwa mama, naye alikuwa akimtafuta huyo mtoto mchanga. Hakuwa akiona hatari hiyo, haikuleta tofauti yoyote, alikuwa akimtafuta mtoto huyo mchanga.

205 Nikageuza kichwa changu, nisingeweza kuliangalia. Nikageuza kichwa changu, nikasema, "Baba wa Mbinguni, mrehemu Bert. Usimwache afanye hivyo, Mungu. Mama huyo wa thamani akiwa amesimama hapo huku moyo huo mnyenyekevu kweli ukidunda hapo chini, akimtafuta mtoto wake mchanga, usimwache afanye hivyo, Baba." Nami nikaendelea kusimama hapo, nikiomba kimoyomoyo. Nilikuwa nimetega masikio nisikie bunduki hiyo ikifyatuka dakika yoyote, lakini bunduki hiyo haikufyatuka.

206 Baada ya kama dakika moja ama mbili kamili, niligeuka, nao mtutu wa bunduki ulikuwa ukitikisika *hivi*. Ndipo akaniangalia, nayo machozi yalikuwa yakitiririka kutoka kwenye hayo macho. Akaniangalia, huku midomo yake ikitetemeka, akaitupa bunduki ukingoni, akasema, "Billy, nimetosheka nayo." Akanishika kwenye mguu wa suruali, na kusema, "Niongoze kwa huyo Yesu unayenena habari zake." Yeye ni shemasi—yeye ni shemasi katika kanisa la Kibaptisti.

207 Kuna nini? Ilikuwa ni kitu gani? Aliona kitu halisi. Aliona kitu ambacho hakikuwa cha kuigiza. Aliona kitu ambacho kilikuwa ni halisi, mama halisi, kitu fulani ndani, hata hakuogopa kifo, hakuogopa chochote, kwa sababu alikuwa ni mama, mtoto wake alikuwa na hitaji. Mungu, nifanye Mkristo kumpenda Bwana wangu, kama yule mama alivyokuwa . . . mama kadiri alivyokuwa mama, nifanye mimi, Mkristo.

208 Vichwa vyetu vikiwa jinsi vilivyo sasa, huku macho yetu yakimwelekea Mungu, ni wangapi humu ndani wangetaka kuwa Mkristo wa namna hiyo, Mkristo kama yule kulungu alivyokuwa mama? Je, ungesema, "Mungu, kuwa . . . " Na tuinamishe vichwa vyetu.

209 Baba wa Mbinguni, nadhani, nitaikumbuka hiyo hadithi kwa muda mrefu. Ninakumbuka nikihisi mikono hiyo ya Bert, alipoushika mguu wa suruali yangu, akinivuta, huku machozi yakitiririka kwenye theluji hiyo nyeupe. Uso wake ulikuwa umembadilisha, alikuwa ameona kitu ambacho kilikuwa halisi, alitaka kuwa Mkristo. Na pale kwenye ukingo huo wa theluji siku hiyo, mtu katili mwenye moyo wa jiwe aliyeyuka, kwa sababu kwamba aliona kitu halisi.

210 Malkia wa Sheba aliona kitu halisi, akashawishika. Yule mwanamke kisimani, aliona kitu halisi, akasema, "Bwana, naona kwamba Wewe ni Nabii. Tunajua Masihi yuaja." Aliona

kitu halisi. Filipo aliona kitu halisi. Bartimayo aliona kitu halisi macho yake yalipofunguka, Mtu ambaye angeweza kuyafungua macho yake yaliyopofuka.

211 Mungu, tujalie, usiku wa leo, tumwone Yesu, tuone nguvu Zake zinazobadilisha maisha yetu kutoka wenye dhambi kuwa Wakristo, kutoka kwa wasioamini, na wenye kushuku, na wenye kushuku wakawa Wakristo waaminio wa kweli wasioghoshiwa.

212 Bariki kila moyo uliokuwa chini ya mikono hiyo iliyoinuliwa. Jalia wasiwe na raha. Jalia wawe kwenye mafungu baridi ya theluji pia, mpaka wafikie ufahamu huo ya kwamba Mungu amewafanya Mkristo halisi mioyoni mwao, kumpenda Mungu mbele za mauti, mbele za chochote, Kristo ndiye wa kwanza, wito wa Mungu na Neno Lake. Tujalie, Baba wa Mbinguni.

213 Tutangojea sasa, na kutumaini ya kwamba Wewe, mpaka wito huu wa madhabahuni utakapomalizika, utajifanya halisi sana kwetu hata tunaweza kuondoka hapa, usiku wa leo, kama yule malkia wa Sheba, akirudi kwenye nchi yake mwenyewe, alishawishika kulikuwa na kitu halisi. Bert, akitoka mwituni, kulikuwa na kitu halisi. Petro hakutaka nyavu zake tena, kulikuwa na kitu halisi alichokuwa ameona.

Mungu, tujalie usiku wa leo, kwamba tutaona kilicho halisi pia na kutambua ya kwamba ni Kristo miongoni mwetu. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

214 Kila ninapowazia juu ya maskini, maskini hadithi hiyo, huko juu, ya yule mama kulungu! Sijui kilichompata. Bert akaanza kupiga mayowe, kwa sauti yake yote, nikainua macho yangu, na hayo macho ya mjusi yalikuwa yamebadilika yakawa uso mzuri, midomo yake ilikuwa ikitetemeka, mikono yake imeikumbatia miguu yangu, akasema, “Niongoze, Billy, kwa huyo Yesu.”

215 Mnaona, ingawa makanisa na kadhalika aliyokuwa akiyatembelea yalinyamaza, miamba iliweza kupaza sauti. Maisha ya huyo mama kulungu yalikuwa yamepaza sauti kwamba yeye...kulikuwa na kitu halisi, kitu ambacho hakikuwa tu ni kuadibishwa kikanisa, kilikuwa ni kitu fulani kilichokuwa halisi, ambacho hakikuogopa, ambacho kilikuwa ni cha kweli.

216 Mungu jalia, usiku wa leo, ya kwamba Bwana na Mwokozi wangu, Yesu Kristo, atajifanya halisi sana kwenu, hata mtaona kitu kilicho halisi, nawe utakuwa mwanafunzi Wake, na uponywe ugonjwa wako.

217 Ninaamini tumeanzia kwenye A, namba moja jana usiku, tukawaita kadhaa. Sijui, nafikiri kuna wengi wao wanaokosekana ambao hatukuwafikia. Hebu tuanzie, usiku wa leo, kutoka mahali pengine.

218 Hebu tuanzie hamsini. A, hamsini. Ni nani aliye nayo? Kadi ya maombi A, hamsini. Vema, labda hiyo pia haipo. [Mtu fulani

anasema, “Papo hapo.”—Mh.] Kwa hiyo tutaanza kutoka mahali pengine basi. Samahani? [“Papo hapo.”] Samahani, mama. Njoo moja kwa moja hapa.

219 A, hamsini. A, hamsini na moja. Papa hapa. Hamsini na mbili, ni nani aliye na kadi ya maombi hamsini na mbili? Naomba uje hapa, ukiweza. Kama hatuwezi, tutakubeba. Hamsini na tatu, inua mkono wako. Hamsini na tatu. [Mtu fulani anasema, “Papo hapo mbele yako.”] Ati mbele yangu? Hamsini na tatu. Vema. Hamsini na nne, ni nani aliye na hamsini na nne? Wewe, bwana. Hamsini na tano. Mtu fulani aliye na kadi ya maombi hamsini na tano ungeweza kusimama? Hiyo ni . . .? La. Hamsini na tano. [Ndugu Branham anakohoa.] (Samahani.) Hamsini na tano.

220 Sasa, itatubidi kuharakisha. Tutachelewa tena. Hamsini na tano. Iseme katika Kihispaniola, mtu anayeweza kuzungumza Kihispaniola. [Mtu fulani anasema, “Cincuenta y cinco.”—Mh.] Hamsini na tano. Huenda alitoka nje. Vema. Wakiingia, kumbukeni, wakati huu, wanaweza kuingia mstarini. Hamsini na sita, hamsini na saba. Vema, asanteni. Hamsini na nane, hamsini na tisa, sitini, sitini, sitini.

221 Sababu ya sisi kufanya hivi, kusudi wasiwe wanakimbia, wakisukumana juu ya mmoja, mwingine. Sitini haipo hapa? Loo, naam. Sitini. Vema. Sitini na moja, sitini na mbili. Hilo ni jema. Sitini na mbili. Inua mkono wako ili tuweze kukuona, unaona. Sitini na mbili, sitini na tatu, sitini na nne, sitini na tano. Hiyo ni kweli, hiyo ndiyo njia ya kufanya hilo. Sitini na tano. Chukua tu kadi yako, na umpe bawabu, ama nanii . . . ama Billy, ama baadhi yao huko chini. Sitini na tano, sitini na tano. Sitini na sita. Vema, sawa.

222 Tafadhali usichukue kadi isipokuwa unataka . . . kama wewe ni . . . Unaona, u—unamwondosha mtu mwingine, mtu fulani kuja . . . Labda nilihubiri kwa muda mrefu kidogo, wananinii . . . inawabidi kwenda nyumbani. Labda ni kosa langu, samahani, huenda ikawa, nilihubiri kwa muda mrefu sana. Vema.

223 Sasa, ni wangapi wasio na kadi za maombi nanyi mnataka Bwana awaponye, nawe unaamini ya kwamba Yeye atakuponya? Inua mkono wako. Vema. Amini tu sasa. Usiwe na shaka, amini.

224 Mnakumbuka kulikuwako na maskini mwanamke mmoja, wakati mmoja, aliyegusa upindo wa vazi Lake, naye pia hakuwa na kadi ya maombi, bali Yeye aliangalia kote mpaka akamwona. Ni wangapi waliokuwa hapa jana usiku? Hebu tuone mkono wako. Vema, nadhani ninyi nyote mlikuwa hapa, mlielewa kilichotukia.

225 Sasa, waweza kusimama kidogo, mama? Sasa, nadhani mimi na wewe hatufahamiani. Labda tulizaliwa tukiachana umbali wa maili nyingi na kuachana kwa miaka kadhaa. Wewe ni msichana tu, na—nami ni mtu wa makamu. Hii ni mara yetu

ya kwanza kukutana, nadhani. Sisi . . . [Dada huyo anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Ulikuwa katika mmoja wa mikutano yangu ulipokuwa mdogo. Na hiyo ilikuwa hapa California? [“Huko Oregon.”] Ati wapi? [“Huko Oregon.”] Huko Oregon. Labda huko nyuma katika huduma yangu ya mwanzoni?

226 Vema, ni . . . Sikujui, bila shaka, kwamba . . . ninii tu, umeniona tu. Naam. Nimeona mamilioni ya watu tangu wakati huo, na nimekuwa . . . Kamwe nisingemkumbuka mtu yeyote kama huyo kwa vyovyote vile. Jambo lingine, nisingejua shida yako, ama . . . Hebu tuone tu kama Bwana ataniambia shida yako basi, ama, tuachane tu na jambo lingine lolote, shida tu. Je, ingekushawishi ya kwamba—ya kwamba . . . Ungejua kama ninakwambia kweli au la, sivyo?

227 Je, ingeshawishi hili kusanyiko? Ungeamini ungeona kitu halisi? Huyu hapa msichana mwenye . . . sote wawili . . . Sasa, sijui ana shida gani, anajua, maana . . . Yeye ni msichana tu aliyesimama hapo. Mtu fulani, yule mvulana hushuka huku, anasambaza kadi hizi za maombi. Nao watu wako huko nje wakiwa na—na kadi ya maombi, ama bila kadi ya maombi, haijalishi, wana imani tu. Hiyo tu ndiyo unayopaswa kuwa nayo.

228 Na sisi hapa, na huyo msichana ana shida fulani. Kama ipo, basi kama Roho Mtakatifu ataifunua, kama hilo si jambo lile hasa ambalo Yesu alikihukumia kizazi hicho! Ndilo hasa. Na jambo lile lile aliloahidi, kama jana usiku, kwa ajili ya kizazi hiki, na kusema kunena dhidi yake kungekuwa ni kumkufuru Roho Mtakatifu, na kamwe mtu hatasamehewa.

229 Sasa, hili hapa. Sasa, jambo fulani halina budi kutukia. Hapa ndipo tunapoweza kusema . . . Katika kusafiri, ni—nilikaribishwa, alasiri moja, huko India katika hekalu la Wajaini, ambapo dini kumi na saba mbalimbali mle ndani, kila moja yazo inaupinga Ukristo, kila moja yazo, Buddha, Mwislamu, hao wote, inaupinga, Kalasinga, Jaini, na *kadhalika* walikuwa mle ndani, nao kila moja iliupinga Ukristo, lakini kila dini ulimwenguni ni ya uongo isipokuwa Ukristo.

230 Kila mwanzilishi amekufa. Buddha alikufa yapata miaka elfu mbili mia tatu iliyopita. Mohammed, alikufa baada ya Kristo. Ndipo tu—tunaona waanzilishi hawa wote wamekufa. Confucius pamoja na falsafa yake, na wote mbalimbali, wamekufa. Waanzilishi wao wamekufa, ila Kristo alikufa na akafufuka tena, yu hai milele.

231 Dini yetu humtoa Mtu aliyeianzisha, Ukristo, Naye yuko hapa pamoja nasi. Hakuna kitu kinachoweza kumwua, Yeye yu hai milele na alisema, “Kazi nizifanyazo . . . Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, ninii . . . ombeni mtakalo, nanyi mtapewa. Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya.”

232 Sasa, kama Kristo angesimama hapa, usiku wa leo, akiwa na suti hii aliyonipa, naye alikuwa amesimama hapa, na huyo mwanamke ni mgonjwa, kama—kama Yeye angeninii . . . angeweza kumponya? Sasa, kuwa mwangalifu sasa kabla hujasema, "Amina." Angeweza kumponya? La, bwana. Angesema tayari alikuwa amefanya hivyo. Hiyo ni kweli? Hakika. "Mtoto wangu," Yeye angesema, "Tayari nimefanya hivyo, kwa kupigwa Kwangu wewe uliponywa. Hivi huamini hili?" Unaona? "Limetekelezwa tayari." Mnaona?

233 Asingemponya, tayari amemponya. Huenda akafanya jambo fulani kumthibitishia ya kwamba ilikuwa ni Yeye. Mnaona? Naye angefanya hivyo kwa njia ile ile aliyofanya *huko* nyuma kuthibitisha *huko* nyuma ya kwamba ilikuwa ni Yeye. Hiyo ilikuwa ni kweli? Sasa, Yeye alilithibitishaje? Tuliyapitia jana usiku, niliyakwepa usiku wa leo, kwa ajili tu ya Sulemani, lakini sasa, kesho usiku, labda tutaliingilia tena.

234 Sasa, angalieni, Yeye—Yeye angelifanya vivyo hivyo, kwa sababu hawezi kufanya uamuzi mwingine, tayari amefanya uamuzi, na huo ndio wa mwisho wa Mungu. Kile Mungu asemacho mara moja, Yeye daima hubaki yeye yule. Hiyo ndiyo sababu unaweza kuliamini Neno, halibadiliki kamwe.

235 Sasa, kama Roho Mtakatifu atakuja juu yangu, na . . . Ni karama tu, siwezi kuifanya itende kazi. Ina . . . ni . . . siiendeshi, inaniendesha. Mnaona? Nayo imani yako itabidi ifanye hivyo. Unaona? Mimi . . . Kama haijalishi angenifanyia nini, inahitaji imani yako kufanya hivyo. Kama vile alivyomwambia yule mwanamke, "Imani yako imekuokoa." Mnaona? Hiyo—hiyo ndiyo njia Yake ya kufanya jambo hilo. Hiyo ndiyo njia . . . Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, na hivyo ndivyo Yeye—Yeye anavyotenda kazi, ni vile vile. Hawezi kubadilika, Yeye daima ni Mungu.

236 Na sasa, njia pekee . . . Kama angekwambia hili . . . Sasa, kama nikija na kusema . . . ulisema, "Ndugu Branham, mimi ni mgonjwa," niseme, "Vema, njoo hapa." Niweke mikono yangu juu yako. "Mungu asifiwe. Biblia ilisema 'Ishara hizi zinafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya.'" Hilo lingekuwa sawa. Labda, kama vile Ndugu Roberts, ama baadhi yao walio na ile imani halisi ya kutishia, waishike. Huyo ni Ndugu Roberts, siwezi kupachukua mahali pake, hawezi kupachukua pangu. Mnaona? Sisi ni wahudumu wawili tofauti, karama mbili tofauti. Mnaona?

237 Lakini kama ningekwambia, "Naam, kama wewe ni mgonjwa, nitaweka mikono yangu juu yako, utapata afya," sasa, kama ukiamini, ungepona. Lakini vipi kama Kitu fulani kinasimama hapa na kukwambia nini kibaya? Unaona? Yaliyokuwapo, na yatakayokuwapo? Ndipo wewe . . . Ni vigumu kutilia shaka hilo, sivyo? Una kitu cha kushikilia. Hiyo ni kweli.

238 Sasa, unakabiliwa na upasuaji, hiyo ni kweli, na huo ni uvimbe. Unaamini Yeye anaweza kuniambia uvimbe ulipo? Ingekusaidia? Uko kwenye tumbo. Unaamini ya kwamba haitakubidi kuwa nao, nao utatoweka? [Mwanamke huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Basi kamwe usitie shaka. Na iwe hivyo, katika Jina la Bwana Yesu.

239 "Kama utaamini!" Sasa, nenda kamwulize huyo msichana, chochote alichoambiwa, mwulize kama alinijua, ama chochote kulihusu, mwulize alichoambiwa, uone kama ni kweli ama si kweli. Mnaona?

240 Sasa, kama kamwe atabaki, shida yoyote aliyokuwa nayo, kama kamwe atabaki na imani hiyo ambayo. . .Niliona Nuru hiyo ilimwangukia tu, nacho kile kivuli cheusi kilichokuwa kimening'inia pale kikatoweka. Unaona? Sasa, kama kamwe atadumu na imani hiyo, wala hataiachilia, atapona. Asipofanya hivyo, basi itabidi jambo lingine, kutukia. Mnaona? Sininii. . . Mimi si mponyaji, Mungu ndiye Mponyaji, na imani yako katika yale Mungu aliyokufanyia tayari. Unaona?

241 U hali gani? Sasa, hatufahamiani, Mungu anatujua sote wawili. Lakini hivi unaamini ya kwamba Mungu angeweza kunifunulia jambo fulani la—la maisha yako, ingeninii. . . kitu kama yule mwanamke ambaye ndio kwanza awe hapa? Ingekuwa. . .?

242 Hapa tena, kama tu vile Bwana wetu alivyokutana na yule mwanamke kisimani, watu wawili, mwanamume na mwanamke walikutana kwa mara ya kwanza maishani, basi hili hapa tena, mwanamume na mwanamke wanakutana kwa mara ya kwanza maishani. Nasi, kwa kuwa hatufahamiani, basi kama. . . Kama kungekuwako na njia yoyote ulimwenguni ningefanya kukusaidia, wala nisingefanya hivyo, nisingestahili kusimama nyuma ya Biblia hii *hapa*, kama ningeweza kukusaidia wala nisingefanya hivyo. Mnaona? Nisingeweza kujiita m—mtumishi wa Kristo.

243 Na kama. . .Huenda ukawa mgonjwa sana madaktari wamekukatia tamaa. Huenda ukawa, umesimama hapo kwa ajili ya mtu mwingine, Huenda ikawa ni ya kifedha, huenda ikawa ni matatizo ya kinyumbani, si—sijui, wewe ni mtu tu aliyesimama hapo, bali Yeye anajua. Na kama Yeye atanifunulia, itakusaidia? [Mwanamke huyo anasema, "Ndiyo, ingenisaidia."—Mh.] Vema. Nitazame basi.

244 Sasa, sababu ya mimi kusema hivyo, Petro na Yohana walisema langoni. . .Sababu ya kusema hivyo, nilihisi Hilo likiingia. Unaona? Unaona? Unaona? Kama vile Petro na Yohana langoni walivyosema, "Tutazame sisi." Unaona? "Tutazame sisi." Wakaangalia kwa bidii kana kwamba. . .

245 Naam, kuna jambo fulani kuhusu damu. Ninamwona huyu mwanamke akitema damu. Ni henia kwenye. . .kutoka kwenye

ini, na—na mishipa ya damu, nayo inajaa ndani yako, nawe huna budi kuitema, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukuponya huo?

246 Roho yeye yule aliye hapa, unajua kuna Kitu fulani kinachonitia mafuta kukwambia; unajua kama ni kweli ama si kweli. Unaamini basi, ya kwamba hiyo . . . ya kwamba mimi ni mwaminio? Unaamini kwamba ni Mungu? Haina budi kutoka kwenye Chanzo fulani. Unaamini kwamba ni Mungu? Basi njoo hapa, na uache tu, nikuwekee mikono.

247 Sasa, Baba, ni kati ya uzima na mauti, jalia Roho wa Uzima amponye mwanamke huyu katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Usitie shaka, nenda tu ukiamini kwa moyo wako wote.

U hali gani? Hatufahamiani, nadhani. Sikujui wewe.

248 Sasa, kuna jambo fulani linalotukia, kuna na—nanii . . . mtu fulani humu ndani anayeonekana tofauti na mwanamke huyu, anaomba, imani kuu sana, inaendelea kuja kati yangu na mwanamke huyu. Ni mtu anayeonekana tofauti, nitampata katika dakika moja. Mtu fulani anagusa. Yuko moja kwa moja mstarini pamoja na huyu mwanamke, moja kwa moja nyuma yake. Shinikizo kuu la damu ameketi hapo, mama mwenye mvi amevaa kitu cheupe, ameketi hapo akiomba kuhusu shinikizo la juu la damu. Inua mkono wako, kama hiyo ni kweli. Unamwamini Mungu? Vema, basi shinikizo la damu litakuacha sasa.

Mtu aliyeonekana tofauti alikuwa amesimama kati yangu na huyo mwanamke, alikuwa mstarini pamoja naye. Alikuwa na . . .

249 Sasa, ninataka uniamini kabisa . . . kwa moyo wako wote, wakati nikizungumza nawe tu kuona kile Yeye angeniambia. Kile mimi . . . Unasema, "Unafanya nini, Ndugu Branham?" Kuwasiliana na roho yako, kama alivyofanya na yule mwanamke kisimani. Kasema, "Nipe maji ninywe," kisha akaendelea, akizungumza kuhusu dini, na kadhalika, na kuabudu, na mahali pa kunywa maji, na kadhalika. Lakini Mungu daima anabaki Mungu.

250 Unaugua, jambo moja, una wasiwasi sana, dhaifu. Hiyo ni kweli. Udhaifu wako huja zaidi sana alasiri, mara baada ya kumaliza kazi yako, machweo, ama kitu kama hicho, unakuwa dhaifu sana. Hiyo ni kweli. Jambo lingine, una kivimbe unachoombea, kivimbe hicho mgongoni mwako. Na kama unaamini ya kwamba Mungu atakiponya! Unaamini ya kwamba atakiponya? Ulifanyiwa upasuaji, uvimbe. Hiyo ni kweli. Mumeo amekuwa na kiharusi. Hiyo ni kweli. Pauline, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Bibi Pauline Capps, wewe nenda ukiamini kwa moyo wako wote, na Mungu atakuponya.

Usiwe na shaka, amini. Mwamini Mungu kwa moyo wako wote.

251 Unaamini? Yesu aliliangalia kusanyiko na kutambua mawazo yao. Hiyo ni kweli? Kutambua wazo lao. Sasa, "Neno la Mungu," Waebrania 4, "ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, hata ni Mtambuzi wa mawazo ya moyo." Hiyo ni kweli? Naye Yesu *alikuwa* ni Neno. Unaamini hilo? Na Yeye *ni* Neno, nayo Biblia ni Yesu katika maandishi. Na inahitaji Roho Wake kuyahuisha Maneno hayo na kuyafanya Hai tena. Mnaamini hilo? Sasa, kama nyote mtaamini hilo, na kushawishika vivyo hivyo juu ya ushahidi kwamba Mungu aliahidi jambo hilo . . .

252 Mke wako yuko hatarini. Simjui, sijawahi kumwona maishani mwangu. Kidogo yeye ni mnene, na, hiyo ni kweli, naye anaugua, udhaifu na kila kitu, lakini jambo lake muhimu ni kukoma hedhi, mabadiliko ya maisha, yamemfanya kuwa na wasiwasi. Hiyo ni kweli.

Amini tu, na itakuwa sawa, dada, shida zako zote zitatoweka.

253 Mungu Mbinguni anajua sijawahi kumwona mwanamke huyo maishani mwangu. Lakini huyu hapa mwanamke huyu alikuwa hapa, amesimama hapa, nilijua hapana shaka ni mke wake, maana nilimwona nyumbani pamoja naye. Amina. Sasa, yeye anajua hilo. Iweni tu na imani.

Sasa, kamwe usiruhusu mtu yeyote ashindilie chochote masikioni mwako, ndugu.

Amini kwa moyo wako wote sasa, dada.

254 Mwulizeni kama niliwahi kukutana naye ama nilimfahamu. La, bwana, sijawahi kumwona maishani mwangu, na Mungu Mbinguni ndiye hakimu wangu, na *hii* ni Biblia Yake. Lakini mwanamke huyu *hapa* angewezaje kuwa amesimama karibu na mtu huyu *hapa*, na kuwaona wakipitia nyumbani pamoja? Ilibidi awe mke wake. Mnaona? Nilingojea tu mpaka nikawa na hakika kabla sijalisema, kwa sababu wakati mwingine kwa njia hiyo, dhambi inatajwa vivyo hivyo. Mnaona? Lakini niliona huyo kweli alikuwa ni mke wake.

255 U hali gani? Samahani. Nilininii tu—nilininii tu—ilitokea tu niligeuka pale na kumwona mwanamke amesimama karibu na mwanamume huyu, ndipo i—ikanibidi tu kuninii . . . Sina budi kufanya tu jinsi Yeye anavyoniambia, mnaona. Nini . . . ? Kitu halisi, kitu fulani, ninakishika. Sasa, unaugua, naam, dada, unaumwa na kichwa, una maumivu makali sana ya kichwa. Una mzigo moyoni mwako, na huo ni kwa ajili ya jamaa mdogo, ni mwanao, naye yuko katika hali ya kurudi nyuma na ana maambukizi. Hiyo ni kweli, inua mkono wako. Amini sasa kwa moyo wako wote, na Bwana Mungu na akujalie haja yako. Usitie shaka. Ninataka tu kuweka mikono yangu juu yenu mnapopita. Mungu awabariki nyote wawili.

256 Ninaipa imani yako changamoto, ninaipa changamoto katika Jina la Bwana Yesu: Wewe amini ya kwamba Kristo aliye

halisi, Mwana wa Mungu, hajafa, bali Yeye yuko pamoja nasi usiku wa leo.

257 Mnajua kanisa la Kipentekoste lina shida gani? Ndiyo hii: limeona mengi kupita kiasi. Hiyo ni kweli. Wakati mmoja maskini. . .mshairi mmoja alikuwa akienda baharini huko Uingereza. Alikuwa ameandika kuhusu bahari, yale aliyokuwa amesoma katika vitabu. Naye akawazia. . . Akashuka, naye akasisimkwa sana kwa sababu alikuwa anaenda. Ninasema jambo hili, kwa namna fulani nipate kuugutua huo, upako mwingi kupita kiasi hunifanya mnyonge sana, inanibi-. . .nimejiondoa kwake. Na kwa hiyo yeye, akienda baharini kuninii. . .naye akakutana na baharia mzee, mnajua ninalomaanisha, baharia akitoka baharini, naye akasema, "Kwani unaenda wapi?"

258 Akasema, "Loo, mimi. . ." mshairi akasema, "Ninaenda baharini. Nimesoma habari zake, na nimeandika habari zake, nimezungumza habari zake, lakini sijawahi kuiona. Loo, ninataka kusikia harufu ya maji ya chumvi, nataka kuona mawimbi mazuri meupe yakishuka, kuona uakisi wa anga la samawati, kusikia shakwe wakilia!"

259 Ndipo maskini baharia huyo akasokota kiko chake mara chache, na kutema mate, kasema, "Nilizaliwa juu yake miaka sitini iliyopita, wala sioni kitu kinachosisimua sana kuihusu," akatema mate, kisha akaenda zake. Kwa nini? Kwa nini haikumsisimua sana? Alikuwa ameiona sana hata ikawa ya kawaida.

260 Na hiyo ndiyo shida yenu ninyi Wapentekoste, mmeona mengi sana ya Roho Mtakatifu, hata amekuwa wa kawaida kwenu. Jambo moja kama hilo lingewafanya makafiri thelathini ama arobaini elfu kuomba upesi sana huko Afrika. Hiyo ni kweli. Jambo moja!

261 Nitawaambia usiku mmoja kilichotukia. Jambo moja tu dogo lililotukia, niliona—niliwaona wenyeji elfu thelathini wanaovaa blanketi wakivunjilia sanamu zao ardhini na kumjia Yesu Kristo. Nami niliwaona wanawake wamesimama pale, wakiwa uchi kabisa, wakiwa tu na kitambaa kikubwa *hivi* juu yao, na kusimama pale, wala hata hawakujua walikuwa uchi. Nami nikawauliza. . .

Bw. Baxter, Bw. Bosworth, na hao wengine, wakasema, "Ndugu Branham, nafikiri walikusudia u—uponyaji."

262 Nikasema, "Sikumaanisha uponyaji wa kimwili, nilimaanisha unataka kumpokea Kristo." Nao walikuwa na sanamu ndogo zilizonyunyiziwa damu ya wanyama na kadhalika. Nikasema, "Kama ninyi ni waaminifu, zivunjilieni mbali sanamu zenu ardhini." Na ilionekana kama dho—dhoruba ya mavumbi ilitokea, ambapo walivunja hizo sanamu za matope ardhini. Na wakati. . .Nikasema, "Papa hapa mwinulieni Kristo

mikono yenu, na kusema, 'Mungu ambaye angeweza kufasiri, na kumfanya mtu huyu namna *hii*, anaweza . . . ni Mungu huyu wa Biblia.' Amini na uinue mkono wako."

263 Ndipo hao wanawake wakaweka mikono yao chini na kuondoka hapo, walikunja mikono yao namna *hii* wapate kuondoka. Siku chache baadaye walikuwa wamepata aina fulani ya matambara ya kujifunika. Mwenyeji angewezaje kamwe, mwenyeji avaaye blanketi, ambaye hata hajui mkono wa kulia na wa kushoto ni upi, na dakika ile ile anapompokea Kristo anatambua yu uchi, huku wanawake wanaodhaniwa kuwa wamejazwa na Roho wanazivua zaidi kila mwaka? Nielezeeni hilo. Watasimama katika kizazi hiki, katika kizazi hiki, na kukihukumu kizazi hiki. Sisi ni washirikina, na mawazo ya kila namna na kadhalika, ambapo wao ni watoto wa kawaida, kuamini. Amina.

264 Nilifanya hivyo, mnaona, sana . . . kusudi niweze kuwaombea watu hawa wengine. Mengi sana hunifikisha mahali ninakuwa dhaifu sana hata karibu . . . Unasema, "Sivyo ilivyo." Vema, ndivyo ilivyo, kama unajua Maandiko, ndivyo ilivyo. Yesu alidhoofika kutokana na mwanamke mmoja kumgusa, mtu mmoja. Sasa, ni . . . Nisingeweza kumvumilia mtu mmoja, wala hakuna mtu mwingine angaliweza, kama Yeye hakusema, "Nyingi kuliko hizi mtafanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba." Mnaona? Hiyo ni kweli. Danieli aliona ono moja, akasumbuka kichwani kwa siku nyingi.

265 Vema, mtu anayefuata, ama, wewe ndiye mtu anayefuata? Vema, bwana. Hatufahamiani, bwana. Hatufahamiani, lakini Mungu anatujua. Sasa, kusudi tu niweze kurudiwa na upako wa kutosha kuwaombea watu wengine hapa, kama Mungu atanifunulia shida yako, utaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Utaamini. [Mtu huyo anasema, "Ninaamini hata hivyo."—Mh.] Unaamini kwa vyovyote vile, hivyo ndivyo ninavyolipenda. Vema, Kasisi, mhudumu, Bw. Gee, Kasisi Gee, una yabisi kavu. Kama unaamini kwa moyo wako wote, ondoka hapa upate afya. Ponywa katika Jina la Yesu Kristo.

266 Sasa, hilo lilikufanya ujisikie kiajabu sana niliposema yabisi kavu. Sasa, Yeye atapo- . . . Kama anaweza kumponya mtu huyo, Yeye anaweza kukuponya. Ondoka tu moja kwa moja jukwaani, ukisema, "Asante, Bwana Yesu."

267 Ugonjwa wa mgongo, figo. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukuponya? Ondoka tu moja kwa moja jukwaani ukisema, "Asante, Bwana Yesu. Nami na—naamini kwa moyo wangu wote."

268 Vema, njoo msichana, niangalie unapokuja. Wewe ni mtoto tu, ni vigumu kuwa na kisukari na uwe mtoto mdogo namna hiyo. Unaamini Mungu anaweza kukuponya? Unaamini? Unaukubali?

Vema. Ondoka jukwaani ukisema, "Asante, Bwana," na upate afya.

269 Angalia hapa, Mpenzi. Wewe ni mtoto tu, nina mtoto Rebekah hapa nje, yapata tu saizi yako na umri wako. Sasa, una ugonjwa wa tumbo, unakusumbua tumboni mwako, vidonda kutokana na hali ya wasiwasi. Unaamini Mungu atakuponya? Kama unaamini, ondoka jukwaani, nenda ule utakacho, na umwamini Mungu kwa moyo wako wote.

270 Vema. Ulikuwa na kitu kile kile, tumbo lenye wasiwasi. Nenda moja kwa moja jukwaani ukisema, "Asante, Bwana Yesu. Ninakuamini Wewe kwa moyo wangu wote." Usiwe na shaka hata kidogo.

271 Vema. Njoo moja kwa moja hapa, dada. Bila shaka ninakuona ukiegemea pale, mwanamke wa umri wako angekuwa hivyo, lakini hakika kuna kitu kingine tofauti mbali na umri tu wa mama. Ni, naam, moja ya mambo yako makuu ni mishipa. Imekuhangaisha kwa muda mrefu sana. Unaamini huu ndio wakati utakapoponywa? [Dada huyo anasema, "Ndiyo, bwana."—Mh.] Basi kubali uponyaji wako katika Jina la Yesu Kristo, ondoka jukwaani, ukisema, "Asante, Bwana Mungu, ninajua nitakuwa mzima." Amina.

Amini. Sasa mimi . . .

Wewe, kijana mwanamke na mwenye wasiwasi, lakini wako ni wakati tu wa maisha unaokushambulia upate kushikwa na wasiwasi wakati huu. Nenda, amini.

272 Udanganyifu, kila mtu akikwambia, "Jirudie. Hakuna kitu kibaya, na kamwe . . ." Lakini wanadanganya, kuna kasoro, kuna kivuli cheusi juu yako. Naam, bwana. Unawezaje kushuka kupitia . . . Ukishuka kupitia kwenye jengo au kichochoro chenye giza, hapana budi kuwe na kitu ambacho hakika hakina budi kushtua mishipa hiyo kwanza, kabla ya hayo—hayo . . . itaninii . . . utashtuliwa, kwa kawaida usingefanya hivyo. Kuna giza linalokuzunguka, lakini nataka kukwambia sasa, limekuacha wakati ukisimama hapo. Ukitaka ku . . .? . . . nenda ukaamini kwa moyo wako wote, upate afya. Utakuwa mzima, dada, endelea tu. Sasa unaweza kuwa mzima.

273 Vema, unaugua ugonjwa wa wanawake, umeugua kwa miaka mingi, na moja ya mambo yako makuu, unahofia utalemazwa na yabisi kavu. Kama ukiamini kwa moyo wako wote, *kamwe* hutalemazwa na yabisi kavu. Nenda ukamwamini Mungu na upate afya.

274 "Na malkia wa Kusini atasimama katika Hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, na kuwahukumu kwamba wamekosa, kwa maana alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili aone hekima ya Sulemani; na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani." Roho Mtakatifu yupo hapa, Roho Mtakatifu, Mungu wa Mbinguni, Bwana Yesu aliyefufuka yupo hapa.

Mnaamini hilo? Jaribuni kulitikisa litoke kwenye moja ya nia zao wale ambao wamekuwa hapa mbele Zake, na mtafute kujua. Waulizeni jinsi walivyojisikia walipopitia hapa, wakiitazama ile Nuru ikiwakalia.

275 Umewahi kuona picha Yake? Ile ambayo sayansi imepiga picha? Kama hujaiona, Bw. Wood anazo huko nyuma, nadhani unazo. Ndugu Wood, uko wapi? Nadhani angali anazo hizo picha. Iko papo hapo. Ni hakinakili kutoka kwa George J. Lacy, mkuu wa FBI. Imetundikwa kwenye Ukumbi wa Sanaa wa Kidini, Kiumbe pekee cha kimbinguni kilichowahi kupigwa picha.

276 Sasa, angalieni. Ni kitu gani kilichowaongoza wana wa Israeli kutoka Misri? Nguzo ya Moto. Hiyo ni kweli? Ni wangapi wanaojua ya kwamba Huyo alikuwa ni Kristo? Bila shaka, ilikuwa ni lile—lile agano . . . Malaika wa agano, alikuwa ni Kristo. Ndipo, alipokuwa hapa duniani, Yeye alisema, "Nimetoka kwa Mungu, naenda kwa Mungu." Hiyo ni kweli?

277 Baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka, na kupaa, tunaona ya kwamba Sauli wa Tarso alikuwa akienda zake kukamata kundi la watu waliokuwa katika njia hii. Basi akienda zake barabarani, Nuru kubwa mno, Nguzo ya Moto, ikamwangusha chini, ndipo akasimama, Naye akasema, "Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?"

Akasema, "U nani Wewe, Bwana?"

Akasema, "Mimi ni Yesu. Nimetoka kwa Mungu, narudi kwa Mungu."

278 Hii hapa Nuru ile ile. Haleluya! Kitu gani? Yesu yeye yule jana, leo, na hata milele. Ni kitu gani? Inafanya jambo lile lile. Huyo kwanza alikuwa Mungu juu yako, kisha Mungu pamoja nawe katika Mwanawe, sasa Mungu ndani yako katika Roho Mtakatifu, Nguzo ile ile ya Moto, iliyothibitishwa na wanasayansi, iliyothibitishwa hapa miongoni mwenu, kwangu mimi ni halisi na la kweli kama upendo wa yule mama kulungu. Ni Mungu halisi wa Biblia, ni halisi, thibitisho la siku za mwisho.

279 Tuko hapa katika huo Uwepo tumefufuka, na katika Uwepo wa Yesu Kristo pamoja Naye katika kufufuka Kwake, kwa kuwa tumeshutumu kutokuamini kwetu. Tunaamini ya kwamba Neno la Mungu ni kweli, Naye yupo hapa akilithibitisha na kulihakikisha kwamba ni kweli. Unaamini hilo?

280 Je, umewahi kumkubali kama Mwokozi wako? Je, unamjua kama Mwokozi wako? Kama jina lako limeandikwa kwenye kitabu cha kanisa, na hilo tu ndilo unalojua, liache hilo mahali lilipo, bali njoo hapa na umjue Yeye.

281 Unasema, "Mimi ni mwanafunzi wa Biblia, lakini kamwe sijawahi kuzaliwa mara ya pili. Sijui chochote kuhusu Roho Mtakatifu." Usininii . . . Sio, "kujua Kitabu Chake ni Uzima,"

bali, "kumjua Yeye." Mjue Yeye, sio Neno, Yeye. Shetani anakijua hicho Kitabu. Bila shaka.

282 Jamaa fulani aliniambia wakati mmoja, nilikuwa nikizungumza juu ya usalama wa mwaminio, akasema, "Huijui Biblia yako."

283 Nikasema, "Lakini ninamjua Mwandishi wake." Hilo ndilo jambo muhimu, ninamjua Mwandishi, "Kumjua Yeye ni Uzima." Hiyo ni kweli. Na kama humjui, mbona usije hapa sasa na kusimama papa hapa katika Uwepo Wake?

284 Sasa, unajua nisingefanya hivyo isipokuwa Roho Mtakatifu alikuwa akiniambia kuna watu humu ndani wanaopaswa kufanya hivyo. Kama vile tu anavyoijua mioyo ya watu, Yeye anajua hali yako. Jichunguze tena, uone kama Maisha ya Kristo yanajiakisi Yenyewe katika mwenendo wako wa kila siku, chunguza.

285 Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa, kwa muda kidogo tu, ninahisi ya kwamba hili ni muhimu. Uliinua mkono wako muda mfupi uliopita ungetaka kuwa Mkristo, Mkriso kadiri yule kulungu alivyokuwa mama. Kama unataka jambo hilo, na kweli unamaanisha kwa moyo wako wote, nawe ulimaanisha hilo, mbona usije huku juu na kulipokea hilo? huku tumeinamisha vichwa vyetu.

286 Kama nilivyosema hapo awali, mimi sipendi sana kuwashawishi watu. Kama Roho Mtakatifu katika kuhubiriwa kwa Neno haleti ushawishi kamili, hakuna haja ya mimi kujaribu chochote changu mwenyewe, maana ninamleta mtu hapo juu chini ya mhemuko. Kama. . .Lakini endapo Roho Mtakatifu Mwenyewe hawezi kukushawishi ya kwamba umekosea. . .Angalia nyuma kwenye Maisha yako, angalia jinsi unavyoishi. Baadhi yenu walei. . .

[Ndugu mmoja ananena kwa lugha, dada mwingine anafasiri. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

. . .katika barabara za Utukufuni na nipaze sauti yangu;

Masumbuko yote yamepita, Nyumbani hatimaye, kushangilia milele.

287 Hivi mtu mwingine hatakuja na kujiunga nao sasa, mtu asiyemjua Kristo; au mtu fulani anayetaka kuomba pamoja nao; mtu fulani asiye karibu vya kutosha na Mungu, ungetaka kufanya upya nadhiri zako tena; mtu asiye na ubatizo wa Roho Mtakatifu? Njoo moja kwa moja huku sasa, wakati maji yanatibuliwa, sasa ndio wakati wa kuingia.

288 Njoni huku, kila mmoja wenu sasa, anayetaka kuja huku na kuomba, anayetaka kusema, "Bwana, nifanye kile ninachopaswa kuwa. Nifinyange tu, ninashuka kwenda kwenye nyumba ya Mfinyanzi, nifinyange tu na kunifanya, Bwana. Nitafanya

maombi sasa. Ninashuka kuja kwenye nyumba ya Mfinyanzi kufinyangwa na kuwekwa sawa, nikishuka kwenda kuvunjwa kwanza, ili niweze kufinyangwa upya."

289 Njoni huku, hiyo ni kweli, sogeeni juu. Kuna nafasi kwa ajili yetu sote karibu na Chemchemi ya Bwana. Yeye yupo hapa, tunajua Yeye yupo hapa, Uwepo Wake upo hapa. Hisia hiyo uliyo nayo moyoni mwako, hiyo ni Mungu, hiyo ni Yeye. Huyo ni Yeye, akitenda kazi, akitekeleza, Roho Wake Mtakatifu tu. Jambo ndilo hilo. Loo, napenda hilo! Shukeni moja kwa moja chini. Hilo ni zuri. Loo, ajabu!

Yesu ni wa ajabu, wa ajabu kwangu,
Mshauri, Mfalme wa Amani, Yeye ni Mungu Mwenye Nguvu;
Loo, kuniokoa, kunilinda na dhambi zote na aibu,
Mkombozi wangu ni wa ajabu, Jina Lake lisifiwe!

Loo, wa ajabu, wa ajabu, Yesu kwangu,
Mshauri, Mfalme wa Amani, Yeye ni Mungu Mwenye Nguvu;
Loo, kuniokoa, kunilinda na dhambi zote na aibu,
Loo, Mkombozi wangu ni wa ajabu, Jina Lake lisifiwe!

290 Sasa, kila mtu, inueni tu mikono yenu sasa na kumsifu, na kumpa Yeye sifa. Mshukuru na Mungu atakuchukua mikononi Mwake . . .?. . .

62-0628 Aliye Mkuu Kuliko Sulemani Yupo Hapa
National Guard Armory
Santa Maria, California Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:



VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org